# KUCHUNGUZA MATUMIZI YA MISIMU YA WANAVYUO INAVYOTUMIKA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII MJINI MOROGORO

**CHRISTINA CLEMENT MALIMA**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA (M.A. KISWAHILI – ISIMU) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapo chini anathibitisha kuwa tasnifu hii iitwayo: "**Kuchunguza Matumizi ya Misimu ya Mugha kwenye Mitandao ya Kijamii kwa Wazungumzaji wa Kiswahili Vyuoni Morogoro"** ameisoma na anapendekeza ikubaliwe na Chuo kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kutimiza sehemu ya sharti ya kutunukiwa digrii ya M.A Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania



………………………………………………

Dkt. Bibiana S. Komunte

(Msimamizi)

……………………………..………

Tarehe

# HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile tasnifu hii kwa ajili yoyote kama vile kieletroniki,kurudufu,nakala,kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

# TAMKO

Mimi **Christina Clement Malima,** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu Kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote.

……………………………..……

Sahihi

………………………………..…

Tarehe

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa wazazi wangu wapendwa Mary Malima na Clement Malima kwa kunipa malezi bora yanayompendeza Mungu na wanadamu pia kwa kuweza kuniwezesha kupata elimu pia mwanangu Anna kwa faraja yake kwangu wakati wa kuandaa tasnifu hii.

## SHUKURANI

Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na vyote kwa kunipa uhai na uzima wa kuweza kukamilisha kazi hii.

Nidhahiri kuwa kazi ya utafiti ni nzito na kukamilisha kwa kazi hii ni kutokana na msaada wa watu wengi hivyo napenda kuwashukuru watu ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine hadi ukamilishaji/kuifanikisha wa kazi hii. Shukrani zangu za pekee zimwendee msimamizi wa kazi hii Dkt B. S. Komunte kwa kukubali kuwa msimamizi wangu na kuwa mshauri wangu mkuu katika kazi hii. Uongozi wa ChuoKikuu Huria Cha Tanzania tawi la Morogoro na makao makuu hasa upande wa M.A Kiswahili kwa ushauri wao kwangu. Shukrani zangu za pekee pia ziwaendee wazazi wangu wapendwa Mary Malima na Clement Malima ambao walinisomesha mpaka nikafikia hatua hii pamoja na kuendelea kujitoa kwangu kama mtoto wao, pia namshukuru sana binti yangu mpendwa Anna pamoja na kuwa ni binti mdogo wa miaka sita lakini alionesha upendo na uvumilivu kwangu katika kipindi chote cha masomo yangu hadi kukamilisha kazi hii. Mwisho, si kwa umuhimu ila kwa nafasi yake ya pekee dada yangu mpendwa Anna Mgassa na ndugu Frank kwa kushirikiana nami na kunitia moyo katika kufanikisha kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia matumizi ya maneno ya misimu ya lugha ya kiswahili na changamoto zake katika mitandao ya kijamii kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Lengo kuu ni kuchanganua matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii na changamoto zake kwa wazungumzaji. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo na sampuli iliyotumika ni sampuli nasibu linganishi kwa kuwa mtafiti alifanya usampulishaji wa watafitiwa kwa kuzingatia na jinsi zao, vilevile eneo la utafiti ni Mkoani Morogoro wilaya za Morogoro mjini na Mvomero. Mbinu zilizotumika kukusanyia data ni usaili, mahojiano, dodoso na ushuhudiaji. Matokeo ya utafiti yameonesha kuwa maendeleo makubwa ya sayansi na teknolojia yamechangia kuongezeka kwa matumizi ya mitandao ya kijamii katika mawasiliano baina ya watumiaji. Vivyo hivyo kumekuwepo na mitindo tofauti ya lugha kwa minajili ya mawasiliano na hivyo kumechangia kutumika kwa misimu ambayo ni lugha isiyo rasmi. Mapendekezo ya watafitiwa kulingana na mada ya utafiti huu ni kuwa maneno ya misimu yanayotumiwa na idadi kubwa ya watu na yanayotumika katika eneo kubwa yanapaswa kusanifiwa. Pia, watu waelimishwe kuhusiana na matumizi ya misimu ili iwe rahisi kueleweka inapotumiwa katika mitandao ya kijamii. Aidha, kuwepo na wataalamu wa uchambuzi wa maneno hayo na kutoa elimu hasa kwa vijana juu ya maana ya jumla na namna yanavyotumika katika mazingira stahiki.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ...................................................................................... ii

**HAKIMILIKI** ...................................................................................... iii

**TAMKO** ...................................................................................... iv

**TABARUKU** ...................................................................................... v

**SHUKURANI** ...................................................................................... vi

**IKISIRI** ...................................................................................... vii

**YALIYOMO** ...................................................................................... viii

**ORODHA YA MAJEDWALI** ...................................................................................... xii

**ORODHA YA VIELELEZO** ...................................................................................... xiii

**ORODHA YA VIAMBATISHO** ...................................................................................... xiv

**ORODHA YA VIFUPISHO** ...................................................................................... xv

**SURA YA KWANZA** ...................................................................................... 1

**UTANGULIZI WA JUMLA** ...................................................................................... 1

1.1 Utangulizi ...................................................................................... 1

1.2 Chimbuko la Misimu ...................................................................................... 1

1.3 Tatizo la Utafiti ...................................................................................... 8

1.4 Tatizo la Utafiti ...................................................................................... 9

1.5 Malengo ya Utafiti ...................................................................................... 10

1.5.1 Lengo Kuu ...................................................................................... 11

1.6 Maswali ya Utafiti ...................................................................................... 11

1.7 Umuhimu wa Utafiti ...................................................................................... 12

1.8 Mipaka ya Utafiti ...................................................................................... 12

1.9 Mpangilio wa Tasnifu ........ 13

**SURA YA PILI ........ 15**

**MAPITIO YA KAZI TANGULIZI ........ 15**

2.1 Utangulizi ........ 15

2.2 Chanzo cha Misimu na Sababu Zake Miongoni mwa Wanachuo katika Mitandao ya Kijamii ........ 15

2.2.1 Misimu ya Lugha ya Kiswahili Katika Mitandao ya Kijamii ........ 17

2.2.1.1 Mapitio ya Kinadharia ........ 17

2.2.1.1 Misimu ya Lugha ya Kiswahili Inavyotumika katika Mitandao ya Kijamii ........ 19

2.2.1.3 Mapitio ya Kisera Juu ya Matumizi ya Misimu ya Lugha ya Kiswahili ........ 21

2.2.2 Changamoto za Kutumia Misimu katika Mitandao ya Kijamii” ........ 22

2.2.3 Kiunzi cha Nadharia........ 22

2.3 Pengo la Utafiti ........ 28

**SURA YA TATU ........ 30**

**MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI ........ 30**

3.1 Utangulizi ........ 30

3.2 Sampuli na Usampulishaji ........ 30

3.2.1 Sampuli ya Watafitiwa ........ 30

3.2.2 Mbinu ya Usampulishaji ........ 31

3.3 Mbinu za Kuchanganua Data Muundo/ Mkabala wa Utafiti ........ 34

3.4 Mbinu na Njia za Kukusanya Data ........ 34

3.4.1 Mbinu ya Hojaji ........ 36

3.4.2 Mbinu ya Usaili ........................................ 36

3.4.3 Mbinu ya Ushuhudiaji ........................................ 37

3.5 Mbinu ya Kupitia Maandiko Mbalimbali ........................................ 38

3.5 Uhalali na Uimara wa Zana za Utafiti ........................................ 38

3.6 Vifaa vya Utafiti ........................................ 39

3.6.1 Shajala na Kalamu ........................................ 39

3.6.2 Kompyuta/Ngamizi/Tarakilishi ........................................ 40

3.6.3 Simu ya Mkononi ........................................ 40

3.7 Changamoto Wakati wa Kukusanya Data ........................................ 41

3.8 Maadili katika Uandishi wa Ripoti ........................................ 41

3.9 Hitimisho ........................................ 42

**SURA YA NNE ........................................ 43**

**UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA MATOKEO YA UTAFITI ........ 43**

4.1 Utangulizi ........................................ 43

4.2 Chanzo na Sababu za Utokeaji wa Maneno ya Misimu kwenye Mitandao ya Kijamii ........................................ 44

4.3 Matumizi ya Misimu Inayotumika Miongoni mwa Wanachuo ..................... 56

4.4 Changamoto za Kutumia Misimu katika Mitandao ya Kijamii Miongoni mwa Wazungumzaji ........................................ 66

4.5 Hitimisho ........................................ 76

**SURA YA TANO ........................................ 77**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........................................ 77**

5.1 Utangulizi ........................................ 77

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Mada ya Utafiti ........................................ 77

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ................................................................ 77

5.3.1 Lengo la Kwanza la Utafiti ............................................................................ 77

5.3.2 Lengo la Pili ................................................................................................ 78

5.2.3 Lengo la Tatu .............................................................................................. 79

5.4 Hitimisho......................................................................................................... 80

5.5 Mapendekezo .................................................................................................. 81

5.5 Maeneo Yanayohitaji Utafiti Zaidi ............................................................... 82

**MAREJELEO ....................................................................................................... 84**

**VIAMBATISHO ................................................................................................... 90**

## ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 3.1: Sampuli ya Watafitiwa .................... 33

Jedwali Na. 3.2: Sampuli ya Watafitiwa Wanachuo kwa Kila Chuo .................... 34

Jedwali Na. 4.1: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kisiasa .................... 45

Jedwali Na. 4.2: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kiuchumi .................... 45

Jedwali Na. 4.3: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kijamii .................... 46

Jedwali Na. 4.4: Orodha ya Maneno ya Misimu Kutokana na Matukio .................... 48

Jedwali Na. 4.5: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake Upande wa Kisiasa .................... 52

Jedwali Na. 4.6: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kiutamaduni .................... 54

Jedwali Na. 4.7: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake Upande wa Kiuchumi .................... 54

Jedwali Na. 4.8: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake Upande wa Kijamii .................... 55

Jedwali Na. 4.9: Majibu ya Watafitiwa kwa Kuzingatia Idadi na Asilimia .................... 57

Jedwali Na. 4.10: Orodha ya Maneno ya Misimu Kulingana na Matukio Tofauti .................... 59

Jedwali Na. 4.11: Orodha ya Maneno Yaliyoandikwa na Idadi Kubwa ya Watafitiwa .................... 61

Jedwali Na. 4.12: Orodha ya Maneno ya Misimu Miongoni mwa Wanachuo .................... 63

Jedwali Na. 4. 13: Orodha ya Maneno ya Misimu katika Kuficha Siri wa Jambo .................... 64

Jedwali Na. 4.14: Orodha ya Maneno ya Misimu katika Kupamba Lugha .................... 65

Jedwali Na. 4.15: Idadi ya Hojaji Zilizojazwa .................... 67

Jedwali Na. 4.16: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake .................... 71

## ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 2.1: Nadharia ya Utafiti........................................................................ 28

Kielelezo 4.1: Dhana ya Msimu Kilaza ....................................................................... 47

Kielelezo 4.2: Misimu Iliyozungumzwa Zaidi 2017 .................................................... 50

Kielelezo 4.3: Dhana ya Msimu Mchepuko................................................................. 69

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na. I: Orodha Hakiki ya Maneno ya Misimu ........................................ 90

Kiambatisho Na. II: Maswali kwa Wahojiwa ............................................................ 99

Kiambatisho Na. III: Orodha Hakiki ya Kupata Maneno ya Misimu ........................ 103

Kiambatisho Na. IV: Maswali kwa Wahojiwa ......................................................... 104

Kiambatisho Na. V: Kibali cha Utafiti (MUM) ....................................................... 105

Kiambatisho Na. VI: Kibali cha Kufanya Utafiti (Mhanda TC) ............................... 106

Kiambatisho Na. VII: Kibali cha Kufanya Utafiti (Morogoro TC) ........................... 107

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TCRA | The Tanzania Communications Regulatory Authority |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Tanzania |
| UKAWA | Umoja wa Katiba ya Wananchi |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| NKM | Nadharia kidhi ya Mawasiliano |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Utafiti huu unahusu kuchunguza matumizi ya misimu ya lugha kwenye mitandao ya kijamii kwa wazungumzaji wa Kiswahili vyuoni Morogoro. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchanganua matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii na changamoto zake kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Katika sura hii ya utafiti imeanza kwa kuelezea chimbuko la misimu, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti ambapo kuna lengo kuu na malengo mahususi, maswali ya utafiti yameainishwa pamoja na umuhimu wa utafiti. Mipaka ya utafiti imeoneshwa na mpangilio wa tasnifu nzima umeainishwa.

## 1.2 Chimbuko la Misimu

Thorne (1990) anaielezea misimu kwa upande wake kuwa hadi mwishoni mwa karne ya 16 matumizi ya misimu yalitamalaki na kuwa kama lugha ya kawaida bila ya kutarajiwa. Thorne (keshatajwa) anaendelea kueleza kuwa kunako karne ya 18 walimu waliwafundisha wanafunzi kutotumia misimu hasa katika lugha ya kiingereza.

Ingawa misimu iliendelea kutumika katika tamthiliya za Richard Brome's na baadaye ikatumika katika mashairi na nyimbo za Cop Land lakini ilipofika miaka 1700 utamaduni tofauti. Ulianza kutumia misimu katika lugha ya kiingereza na misimu kuanza kupanuka. Kwa jumla maneno ya misimu wakati huo yalianza kutumika Uingereza naAmerika. Zaidi ya hapo kulikuwa na matukio kadhaa yaliyotokea katika karne ya 18 yaliyochangia kuendeleza misimu.

Misingi ya kuzuka misimu inakuwa ni ile ile ya kutaka kueleza dhana fulani ambayo imejitokeza katika mfumo wa maisha ya wanajamii katika vipindi fulani kwa mfano njaa, mafuriko, hali ngumu za uchumi, magonjwa na kadhalika. Inaelezwa pia kuwa misimu mingine huzuka kutokana na hali ya utani miongoni mwa watu mbalimbali katika jamii. Mara nyingi, misimu ya aina hii hubeba kebehi, dhihaka,kejeli, mabezo, dharau au kusifu kusiko kwa kawaida.

Chanzo cha misimu kulingana na majibu ya watafitiwa yatajibainisha vizuri kwenye sura ya nne misimu ni mabadiliko ya kihistoria ya jamii katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni ambazo pia zimechangiwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Nyanja hizo zimeweza kuibua maneno ambayo yanaweza kuzuka au kuibuka na kisha kutoweka kulingana na wanavyuo,wakufunzi na wahadhiri mitandaoni. Katika nyanja za kisiasa mabadiliko ya kiutawala yameibua miongoni mwa maneno kama ‘hapa kazi tu’, ‘majipu’, ‘watumishi hewa’ , ‘ruksa’‘vilaza’, ‘ubinafsishaji’ na ‘utandawazi’. Mabadiliko ya kiuchumi yamesababisha kuibuka kwa maneno mbalimbali kama ‘vyuma vimekaza’, ‘kupambana na hali yako’, ‘jero’, ‘dala’ makinikia na ‘buku’. Kwa upande wa nyanja za kijamii na kiutamaduni kumeibuka maneno kama ‘chura’, ‘amsha dude’, ‘jaza ujazwe’, na ‘toa malinda’.Hata hivyo maneno hayo yakiendelea kutumika kwa muda mrefu katika jamii husanifiwa na kuwa maneno sanifu ya lugha. Miongoni mwa hayo maneno ambayo yameshika mizizi ni shangingi, ujasiriamali, ubinafsishaji nakadhalika.

Dhana ya misimu imeweza kufasiliwa na wataalamu mbalimbali kulingana na aina na matumizi yake hali kadhalika na chanzo katika muktadha stahiki. Sengo (1973) anaeleza kwamba misimu huzaliwa katika vikundi vya mikutano ya jamii hasa

mitaani, pia anaeleza kuwa ikumbukwe kwamba vijana hata wasomi na watu wazima waliojitenga katika makundi ya shughuli maalum wote wanatabia ya kuzalisha misemo ambayo haifahamiki na watu wengi katika jamii wanamoishi watu hao.

Zakayo (1998) anaeleza kuwa watumiaji wengine wa Kiswahili hawatumi fursa ya kujua misimu wakidai kuwa ni misemo ya kihuni hasa wakina kabwela na wabwia unga. Kutokana na maelezo yake inadhihirisha kuwa misimu ina umuhimu mkubwa katika mawasiliano miongoni mwa wanajamii walio katika hali ya chini. Thorne (1990), Spears (1991), Champan (1995), Wales (2001) na Dalzell (2016) kwa pamoja wanadai misimu ni lugha ya siri inayozungumzwa na kueleweka na kundi la watu wenye utamaduni mmoja kwa lengo la kujitenga na kundi kubwa la jamii hiyo.

TUMI (1998) Misimu ni maneno yanayoibuka katika kipindi fulani cha historia na hatimaye huweza kupotea. Maneno haya hutumika na kufasiliwa kulingana na kundi mahususi la wanajamii. Ngure (2003) anaeleza kuwa uzukaji wa misimu ni wa ghafla na wakati fulani hufuatana na mambo au matukio maalumu ya wakati au msimu huo. Msanjila na wenzake(2009) wanadai kuwa misimu ni aina ya misemo katika lugha ambayo huzuka na kutoweka. Wanaendelea kusema kuwa kuzuka kwa misimu hutegemea mahitaji ya kikundi hicho kwa wakati huo na mara mahitaji hayo yanapokwisha, basi na misimu hiyo nayo hutoweka.

Nyangwine na Masebo (2010) wanaielezea dhana ya misimu kuwa ni maneno yasiyosanifu yazushwayo na kikundi cha watu wachache wenye utamaduni mmoja ili kuelezea uhusiano wao kama kikundi au kuhusu jamii kubwa ambamo

vikundi hivyo vinaishi katika kipindi fulani cha wakati; na hatimaye maneno hayo hupotea na yanayodumu husanifiwa na kuwa msamiati rasmi wa lugha inayohusika. Wanaendelea kufafanua kuwa simo ni neno mbadala la misimu. King'ei (2010) anafasili kuwa misimu ni matumizi ya lugha ambayo hudhihirisha kiwango cha juu cha ubunifu na mara kwa mara ucheshi. Aidha, King'ei anaeleza kuwa matumizi ya misimu huvunja kanuni za lugha sanifu.

TUKI (2011) anaeleza kuwa simo ni neno au maneno yanayozuka na kutumiwa na watu kwa muda fulani na baadaye hupotea. Halikadhalika, Omari(2009) anaona kuwa misimu ni lugha ya siri. Omari ameweza kubainisha matumizi ya misimu nchini Tanzania na kuona kuwa ni maneno yanyotumiwa sana katika miziki ya kemi(bongofleva).

Baada ya kuangalia dhana ya misimu miongoni mwa wataalamu tajwa hapo juu waliweza kubainisha sifa za misimu kama ifuatavyo;

(i) Huzuka na kutoweka kufuatanana mabadiliko ya jamii.

(ii) Ni lugha isiyo sanifu.

(iii) Ina chuki (kutoelewana) kwani maneno mengi yamebeba kebehi.

(iv) Ni lugha ya mafumbo.

(v) Ina maana nyingi.

(vi) Haidumu muda mrefu.

Nyambari na Masebo (2002) wameigawa misimu katika aina kuu tatu ambazo ni:

(i) Misimu ya pekee hii hueleza mahusiano ya kikundi kimoja kutoka kwenye utamaduni mmoja. Misimu hii hupatikana sehemu moja ya kazi

au mahali waishio watu wa aina moja. Eneo la matumizi ya misimu ya aina hii huwa ni dogo.

(ii) Misimu ya kitarafa hii huchukua eneo kubwa au pana kimatumizi misimu ya aina hii huweza kupatikana kwenye kata, tarafa, wilaya, Mkoa watu waliopo katika kundi hili wanamchanganyiko wa tamaduni.

(iii) Misimu zagao hii huenea nchi nzima au kuvuka mipaka ya nchi. Misimu zagao hutumika katika mikoa yote mbalimbali na vilevile hutumika katika magazeti,vitabu na katika vipindi vya radio. Mfano wafurukutwa, wakereketwa, wapambe, vilaza n.k

Licha ya kuangalia aina za misimu, pia misimu huwa na dhima zifuatazo:

(i) Hutumika kupamba lugha

(ii) Hutumika kukuza lugha

(iii) Hutumika kutunza historia ya jamii fulani

(iv) Hutumika kuibua hisia mbalimbali za wazungumzaji

(v) Hutumika katika kufurahisha na kuchekesha.

Matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii ni suala ambalo limeikumba jamii katika kipindi hiki cha maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika kuelezea dhana hii haina budi kuelewa maana ya mitandao ya kijamii.

Mitandao ya kijamii ni aina ya tovuti au aplikesheni zinazowaruhusu watumiaji kuwasiliana kwa kuchapisha na kutumia jumbe za maandishi, picha, video, kwa kutumia kompyuta au simu za mkononi. Mitandao ya kijamii huwaleta watu pamoja ambao hujadili mada mbalimbali zinazohusu masuala ya kisiasa, kijamii, kiuchumi,

kiutamaduni ambapo inahusisha dini, elimu nahata mada zinazohusu utandawazi kwa jumla. Mitandao ya kijamii imerahisisha sana mawasiliano ambapo kwa muda mfupi mtu anaweza kusambaza mada au ujumbe wowote duniani kote. Mitandao hiyo imefasiliwa kama ifutavyo:

Facebook ni aina ya mtandao wa kijamii unaowaruhusu watumiaji wake kuchapisha na kutumiana taarifa kwa njia ya maandishi, picha au video. Mtandao huu unawaruhusu marafiki kutafuta marafiki wanaotumia mtandao huo kokote duniani kwa ajili ya kubadilishana nao mawazo juu ya masuala mbalimbali yanayohusu biashara, siasa, dini nakadhalika.

Whatsapp ni mtandao wa kijamii maarufu duniani unaowaruhusu watumiaji wake kutumiana jumbe za kimaandishi, sauti, picha, video pamoja na kupiga simu kwa sauti au kwa kuonana kwa kutumia intaneti. Ili mtu aweze kutumia mtandao huu anatakiwa awe na namba ya simu ambayo itatambulika kwenye mfumo wa whatsApp kama jina la mtumiaji. Matumizi ya mtandao wa whatsApp inampasa mtu kuwa na kifaa chenye uwezo wa kutumia whatsApp, Facebook Na mitandao mingine kwa kutumia simu-janja au tablets pamoja na line za simu za mkononi. Mtumiaji wa whatsApp ana nafasi ya kumtumia mtu mmoja taarifa au kundi la watu kwa wakati mmoja. Mawasiliano katika mitandao yalianza takriban miaka 40 iliyopita historia ya mitandao ya kijamii inaweza kuangaliwa kuanzia mwaka 1994

Tweeter ni mtandao unaokuwezesha kuandika ujumbe mfupi wa maneno usiozidi maneno 140 na kushirikisha watu wengine. Ujumbe huo wa maneno 140, huitwa ‘tweet’ na kitendo cha kuandika na kurusha hewani tweet yako ndio huitwa “ku

tweet" na pia unaweza kushare tweets za watu wengine kitendo hicho huitwa ku retweet. Ili uweze kujiunga na mtandao huu unatakiwa uwe na anwani ya barua pepe kisha unaingia kwenye website ya tweeter (www.tweeter.com). Istagram ni mtandao wa kijamii kama mitandao mingine ambao unaweza kutoa picha na video zake na kushirikishana na marafiki, ndugu na jamaa.

Timothy (2016) katika tasnifu yake kuhusu maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii husan facebook na tweeter anaeleza kuwa Mitandao ya kijamii kupitia habari, picha na video huwasaidia watumiaji kuungana pamoja na kujipatia marafiki wapya na kuendelea kuwasiliana nao kwa kutumia mtandao wa intaneti. Kupitia mitandao hiyo watu hujenga mfumo wamtandao na marafiki ambao huweza kufikia maelfu na maelfu ya watu.

Mitandao ya kijamii inaonekana imekuwa na watumiaji wengi sana katika kipindi cha miaka michache iliyopita ambayo imewahusisha vijana, wanasiasa na wafanyabiashara. Anaendelea kusema kuwa watumiaji wa mtandao huu huweza kujadili kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiutamaduni, kuwasiliana na kuuza au kununua bidhaa zao katika mtandao. Maendeleo ya kiteknolojia yamekuwa ndio chanzo kikubwa cha kuzinduliwa kwa mitandao mingi ya kijamii. Kiunga, anaona kuwa malengo ya mawasiliano katika mitandao ya kijamii ni kuleta utangamano baina ya wanajamii. Vilevile, kupitia mitandao ya kijamii watu huelewana kwa urahisi kwa sababu huwa wamejipanga katika makundi mbalimbali. Mfano, watu walio katika taaluma moja au kufanya kazi eneo moja hivyo huwa rahisi kwao kuelewana.

Maneno ya misimu hutumiwa katika mitandao ya kijamii kama alama ya utambuzi na kushirikishwa maarifa miongoni mwa watu wenye utamaduni unaofanana. Mitandao hiyo ni zao la uvumbuzi na ubunifu wa kisayansi na kiteknolojia. Hivyo (Tellaria 2012 p.2) anadai kuwa mitandao ya kijamii imeruhusu jamii kuibua lugha yake.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Mitandao ya kijamii imechukua nafasi kubwa sana katika mawasiliano ya wanajamii takribani kila siku watu wanaotumia mitandao ya kijamii wanazidi kuongezeka na lugha ndio nyenzo yao kuu ya awasiliano . maneno ya misimu nayo yaeonekana kutuika zaidi miongoni mwa watumiaji wa mitandao ya kijamii. Utafiti wa Kiunga (2016) uliohusu " **maana ya usemi na maungumzo kwenye mitandao ya kijamii hususani facebook na twitter"** Abdallah (2013) amefanya utafiti juu ya misimu ya vijiweni katika lugha ya Kiswahili mifano katika jiji la Dar es Salaam. Tafiti hizi mbili zimegusia suala la misimu na mitandao ya kijamii, mtafiti anataka kubaini nini hasa chanzo cha maneno hayo ya misimu? Yanatuika kwa kiasi gani? Na je kuna rika maalumu ambalo linapenda kutumia maneno hayo ya misimu? Na je maneno hayo yanavyotumika katika mitandao ya kijamii yanaleta changamoto zipi katika mawasiliano? Haya ni maswali yaliyomsukuma mtafiti kutafuta majibu.

Lugha ya Kiswahili ni chombo muhimu sana cha mawasiliano katika mahusiano ya kijamii katika nyanja zote kisiasa, kiuchumi na kijamii. Madhumuni makubwa ya mawasiliano ni kupeleka ujumbe kwa walengwa kwa miktadha mbalimbali. Hivyo ujumbe ukishindwa kufika kwa walengwa kuna kuwa na tatizo na hapa sasa tunagusia maneno ya misimu ni kwa namna gani imeibua changaoto katika mawasiliano kimtandao.

Utafiti huu umebaini kuwa mitandao ya kijamii imekuwa na mchango mkubwa katika kuongeza msamiati wa lugha ya Kiswahili kupitia maneno ya misimu.Maneno hayo ya misimu huweza kueleweka kwa watu maalumu ambao wanaujuzi wa hali ya juu wa lugha kupitia miktadha mbalimbali. TUKI (2013) wanaeleza kuwa simo ni neno au maneno yanayozuka na kutumiwa na watu kwa muda fulani na baadaye hupotea. Misimu/Simo ni maneno ambayo hayajasanifishwa na hutumika zaidi katika mawasiliano yasiyo rasmi.

## 1.4 Tatizo la Utafiti

Tafiti mbalimbali zilizofanywa ambazo zimechunguza kwa undani kuhusu matumizi ya lugha kutokana na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia, katika kuchunguza dhana hiyo Mohamed (2013) amefanya utafiti juu ya Matumizi ya lughatandawazi katika simu za kiganjani; changamoto katika lugha ya Kiswahili. Utafiti umebaini kuwa kuna athari za kiisimu na zisizo za kiisimu zinazoletwa na lugha tandawazi. Abdallah (2012) amefanya utafiti juu ya misimu ya vijiweni katika lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yamebainish misimu ya vijiweni inavyotumika katika lugha ya Kiswahili na maana zake. Pia amebainisha kundi rika ambalo linapenda zaidi kutumia misimu ya vijiweni, na akaainisha faida na hasara za matumizi ya misimu ya vijiweni katika lugha ya Kiswahili. Suala la matumizi ya misimu na mitandao ya kijamii vimesababisha changamoto za kimawasiliano miongoni mwa watumiaji wa mitandao hiyo.

Zipo changamoto za kimawasiliano zinazowakabili wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili kutokana na matumizi ya misimu ya lugha hiyo katika mitandao ya kijamii. Pamoja na mchango wa misimu hiyo katika kukuza misamiati ya

lugha ya Kiswahili, wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu huweza kushindwa kupata maana iliyokusudiwa. Hali inayosababisha kuchangia kutokuelewana vema miongoni mwa watumiaji wa misimu mitandaoni. Mahusiano baina ya matumizi ya misimu hii na changamoto zake kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii kwa lugha ya Kiswahili haijawahi kufanyiwa au kubainishwa waziwazi bali hufikiriwa tu. Kwa mfano maneno ya misimu 'Nitigopesa' likiwa na maana niongezee salio kwenye tigo pesa linatumika sana na wafanyabiashara wanaofanya biashara kwa kutegemea katika mitandao. Neno hili la msimu hutumiwa na kundi la wafanyabiashara na wale wasiojishughulisha na aina hii ya biashara wanaweza wasielewe maana iliyokusudiwa.

Kulingana na dhana za wataalamu mtafiti ameweza kubaini tatizo la utafiti huu kwa kupitia ufafanuzi wa King'ei (2010) anaeleza kuwa misimu huvunja kanuni za lugha sanifu. Kwa hiyo, fasili ya King'ei imebainisha misimu ni tatizo kwani si kila mtumiaji wa mtandao wa kijamii hususani wanavyuo, wahadhiri na wakufunzi huweza kufahamu maana iliyokusudiwa ya maneno hayo ya misimu kwa kuwa maana zake sio za jumla kwa watumiaji wote. Kutokana na tatizo hilo, utafiti huu umekusudia kuchunguza matumizi ya maneno ya misimu na changamoto zake miongoni mwa wazungumzaji hawa.

## 1.5 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti huu yamegawanyika katika sehemu kuu mbili, ambazo zinakamilishana katika utafiti huu. Malengo hayo ni lengo kuu na malengo mahususi.Adam (2008) anaeleza kuwa malengo ya utafiti ni yale madhumuni

yaliyokusudiwa na mtafiti. Malengo hutueleza mtafiti anataka kupata nini mwisho wa utafiti wake.

### 1.5.1 Lengo Kuu

Kuchanganua matumizi ya maneno ya misimu miongoni mwa wanavyuo katika mitandao ya kijamii na changamoto zake.

### 1.5.2 Malengo Mahsusi

Lengo kuu la utafiti hukamilishwa na malengo mahususi yafuatayo:

(i) Kuchunguza sababu za chanzo cha utokeaji wa maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii miongoni mwa wanachuo

(ii) Kuchambua kiasi cha utumiaji wa misimu ya lugha ya Kiswahili inavyotumika miongoni mwa wanachuo.

(iii) Kuchunguza changamoto za kutumia misimu ya lugha katika mawasiliano miongoni mwa wanachuo mitandaoni mfano wasp na istagram

## 1.6 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu utaongozwa na maswali yafuatayo ambayo yatasaidia kufikia malengo ya utafiti:

(i) Sababu zinazopelekea chanzo cha utokeaji wa maneno ya misimu ya wanachuo kwenye mitandao ya kijamii?

(ii) Misimu ya wanavyuo inatumika kiasi gani katika mitandao ya kijamii kwa upande wa istagram na wasapu?

(iii) Ni changamoto gani za kimawasiliano wanazokumbana nazo wanavyuo mitandaoni kutokana na matumizi ya misimu?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) miongoni mwa jamii ya watanzania hasa mijini yamekuwa makubwa hivyo kupelekea kuwepo na matumizi makubwa ya maneno ya misimu. Hivyo, kumekuwa na haja ya kufafanua maana mbalimbali ya misimu ya lugha ili kuwezesha ujumbe uliokusudiwa katika mawasiliano kueleweka. Utafiti huu utasaidia yafuatayo:

(i) Kuweka bayana namna ya kutatua changamoto zinazowakabili watumiaji wa misimu ya lugha katika mitandao ya kijamii.

(ii) Kuonyesha mchango wa maneno ya misimu kwenye mitandao ya kijamii katika kukuza lugha ya kiswahili.

(iii) Utawasaidia walimu na wanafunzi kuwasiliana kwa kutumia maneno ya misimu na hivyo kusaidia kuongezeka kwa msamiati.

(iv) Kuongeza idadi ya istilahi ambazo zitakuwa ni chachu kwa wanaleksikografia wakati wa utunzi wa kamusi.

(v) Utakuwa ni rejeleo kwa tafiti nyingine zitakazofanywa na watafiti watakaofuata.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza maoni ya matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii na changamoto zake miongoni mwa wanavyuo . Utafiti huu pia umewalenga walimu na wanachuo wa vyuo cha Ualimu viwili na chuo kikuu kimoja katika Mji wa Morogoro.

## 1.9 Mpangilio wa Tasnifu

Utafiti huu umegawanyika katika sura tano zinazojengana moja baada ya nyingine. Sura ya kwanza imeelezea utangulizi juu ya utafiti husika ambako kuna chimbuko la misimu, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti ambapo ndani yake kuna lengo kuu na malengo mahususi ya utafiti husika. Pia, kuna maswali ya utafiti na umuhimu wa utafiti umebainishwa bayana. Mipaka ya utafiti na mpangilio wa tasnifu nzima umeelezewa katika sura hii.

Sura ya pili imeelezea mapitio ya kazi tangulizi kuhusu chimbuko la misimu, matumizi yake na changamoto za kutumia misimu. Kwa jumla, mapitio hayo yamekuwa msaada mkubwa kwa mtafiti kuweka wazi tamko la utafiti kwa kudokeza maeneo ambayo bado yalihitaji utafiti unaojitosheleza. Aidha, sura hii imeelezea kiunzi cha nadharia ya utafiti huu kulingana na mada husika. Sura ya tatu inahusu mbinu na vifaa vya utafiti ambavyo vimeainishwa kwa undani, kwani ndizo zana muhimu ambazo zimesaidia utafiti huu kuweza kukusanya data kwa usahihi.

Sura hii imeaanza na usanifu wa utafiti, eneo la utafiti na sababu za kuteua eneo husika ambapo utafiti umefanyika, sampuli na usampulishaji, mbinu na njia mbalimbali zilizotumiwa na mtafiti katika kukusanya data zimefafanuliwa katika sura hii. Uhalali na uimara wa zana za utafiti umebainishwa, pia vifaa vya utafiti vimeainishwa pamoja na changamoto alizokumbana nazo mtafiti wakati wa kukusanya data. Mwisho maadili katika uandishi wa ripoti yamebainishwa. Sura ya nne ni uwasilishaji na uchanganuzi wa matokeo ya utafiti, data zilizopatikana uwandani na maktabani ambazo zote zimechambuliwa kwa kutumia misingi ya

nadharia husika na kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Sura ya tano, ambayo ni ya mwisho katika utafiti huu inahusu muhtasari wa matokeo ya mada ya utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo ya utafiti ambayo yamezingatiwa kwa undani. Adha, sura hii imeelezea kuhusu hitimisho la utafiti mzima.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada inayotafitiwa ambayo inahusu "matumizi ya misimu kwenye mitandao ya kijamii na changamoto zake kwa wazungumzaji wa kiswahili". Vilevile inahusu ufafanuzi wa kiunzi cha nadharia iliyotumika katika utafiti huu.Mapitio ya machapisho haya yataangalia fasili ya misimu kwa ufupi na aina za *misimu* kama zilivyoelezewa na Wales (2001) Thome (1990), Dalzell (2006), Chapman (1995), Spears (1991, 2006).

Wataalamu hao wameeleza kuwa misimu ni lugha ya siri inayozungumzwa na kueleweka na kundi la watu wenye utamaduni mmoja kwa lengo la kujitenga na kundi kubwa la jamii hiyo, wameendelea kueleza kuwa misimu hubadilika mara kwa mara na makundi tofauti ya watu huzungumza misimu yao. Mapitio haya yamegawanyika katika vipengele vitatu, yaani:

(i) Chanzo na sababu za utokeaji wa misimu ya lugha miongoni mwa wanachuo katika mitandao ya kijamii,

(ii) Jinsi misimu ya lugha ya Kiswahili inavyotumika katika mitandao ya kijamii miongoni mwa wanachuo

(iii) Changamoto za kutumia misimu ya lugha ya Kiswahili katika mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii miongoni mwa wanachuo"

## 2.2 Chanzo cha Misimu na Sababu Zake Miongoni mwa Wanachuo katika Mitandao ya Kijamii

Misimu ni maneno ambayo huzuka miongoni mwa kundi fulani katika jamii na hueleweka tu miongoni mwa watu katika kundi hilo. Misimu hukua na kutoweka

baada ya muda. Mitandao ya kijamii katika ni aina tu ya mawasiliano ya kielektroniki inayotumia kompyuta ambapo watumiaji au washiriki hujenga jamii ya kimtandao. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) anasema kuwa misimu ni semi (hata maneno pia) za kimafumbo ambazo huficha maana yake na huhitaji uchunguzi kuitambua. Kimsingi, semi hizi huusishwa na kikundi kidogo cha wanajamii na matumizi yake siyo rasmi. Kikundi hicho hubuni semi hizi ili kuwasiliana wao kwa wao.

Pia tafsiri nyingine ya misimu ni maneno ama misemo ambayo huzuka ghafla katika misimu au wakati fulani, hasa kufuatana na mambo ama matukio maalum ya wakati au msimu huo (Senkoro,1982:25). Ufafanuzi wa mtaalamu huyu hautofautiani sana na wa Balisdya(1987) ambaye anaona misimu kama semi ndogondogo za kupita ambazo huzushwa katika mazingira fulani halafu huja baada ya mazingira yale kutoweka. Semi hizi aghalabu ni za kitamathali. Kutokana na fasili hizo hapo juu misimu imeanza kama misemo au maneno tu yanayoibuka katika kuelezea Chimbuko la misimu ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii limechunguzwa kwa kiasi kidogo. Utafiti wa Kiunga (2016) **“maana ya Usemi Na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii hususani facebook na twitter”**.Mohamed (2013) pia amefanya utafiti juu ya “**matumizi ya lughatandawazi katika simu za kiganjani changamoto katika lugha ya Kiswahili”.** Tasnifu hii ilijikita katika matumizi ya lugha kutokana na utandawazi katika simu za kiganjani na changamoto zake. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kuwa kuna athari za kiisimu na zisizo za kiisimu zinazoletwa na lugha tandawazi, mtafiti ameeleza mtumiaji wa lugha ya Kiswahili ataelewa athari za lugha tandawazi katika Kiswahili na hivyo atakuwa makini na mtindo huu na mingine itakayoibuka katika jamii.

Hata hivyo utafiti huu haukujishughulisha na misimu ya lugha ya Kiswahili, bali ilishughulika na lugha kwa ujumla, hivyo utafiti huu unakusudia kuziba pengo hili. Katika utafiti wa Inocent Shayo (2015) katika utafiti wake alishughulikia ‘‘semi zilizoandikwa katika maeneo ya biashara; uchunguzi kuhusu asili, muundo, miktadha na utokeaji na dhima’’ na lengo la utafiti huo ilikuwa ni kuchunguza asili, matumizi ya lugha na dhima za semi zilizoandikwa katika maeneo mbalimbali ya biashara kama vile kwenye maduka,hoteli, migahawa, sokoni magengeni na vibandani. Na matokeo ya utafiti huo yatasaidia kuonyesha faida, umuhimu na nafasi ya semi ambazo huandikwa katika maeneo mbalimbali ya biashara. Lengo la utafiti huu wa semi ambazo huwa ni maneno yanayoibuka kama ilivyo misimu imesaidia kwa mtafiti kuweza kubaini chimbuko na matumizi ya semi.

### 2.2.1 Misimu ya Lugha ya Kiswahili Katika Mitandao ya Kijamii

#### 2.2.1.1 Mapitio ya Kinadharia

Massamba (2004) katika kuelezea nadharia, anasema kuwa nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo. Kwa mantiki, nadharia huwa ni dira ya kumwongoza mtafiti katika kukabiliana na jambo katika utafiti wake. Utafiti huu ulichambua data kwa kuongozwa na nadharia jumuishi ya Giles (1979) kwa mujibu wa Msanjila na wenzake (2009), nadharia hii hufafanua kwamba utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea, ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamiilugha (kama vile utamaduni, mila na desturi) ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii. Lugha hutumika katika mchakato huu kama ishara muhimu ya kuelezea huo utambulisho unaohusika. Msingi wa nadharia hii

jumuishi unazingatia fasili ya jamiilugha inayosema,"jamiilugha inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanatokana na jamiilugha moja ambayo iko tofauti na jamiilugha nyingine". Fasili hii ya jamiilugha mbali na kuwa msingi wa nadharia hii jumuishi pia ni msingi wa maana halisi ya utambulisho.

Kuna maana halisi mbili za utambulisho, kwanza ni kwa jamiilugha yenyewe kujitambua kuwa iko tofauti na jamiilugha nyingine katika masuala ya msingi kama utamaduni, mila na desturi, imani (dini), chakula, mavazi, uchumi au siasa. Utambulisho wa aina hii ndio msingi wa jamiilugha kutetea na kudumisha amali za jamii yao na ndio msingi wa mtu au jamii kutetea na kusisitiza dhana ya sisi zaidi kuliko wao. Mzungumzaji anapofikia hatua ya kusema hadharani kwamba sisi hatufanyi hivyo, sisi asili yetu ni mahali fulani, lugha yetu sisi ni fulani, chakula chetu sisi ni fulani. Kimsingi anadhihirisha mfungamano uliopo baina yake na jamiilugha yake.

Pili, kwa wanajamii lugha wenyewe kuthamini lugha yao pamoja na vibainishi vingine vya msingi vinavyowafanya wajione tofauti na wana jamii lugha nyingine.

Kwa kuwa misimu hutumiwa na kundi fulani katika jamii lugha yenye kufuata utamaduni, mila na desturi za aina moja, mtafiti ameamua kutumia nadharia hii ili kubaini utambulisho wa kundi hilo. Aidha, utambulisho wa pili umetuwezesha kutambua kuwa jamiilugha ya wanavyuo hudumisha utamaduni, mila na desturi, imani, chakula, mavazi katika mawasiliano yao. Hivyo, nadharia hii inaihusisha zaidi na jamiilugha ili kuweza kudumisha utambulisho wao kati ya jamiilugha moja na nyingine kwa vitendo ili utambulisho wao uweze kudumu.

Vilevile, utafiti huu unaongozwa na nadharia ya Isimu ya Lugha na vipengele vitakavyoongoza utafiti huu ni tawi la Isimu jamii.

#### 2.2.1.1 Misimu ya Lugha ya Kiswahili Inavyotumika katika Mitandao ya Kijamii

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusiana na misimu. Utafiti wa Abdallah, (2013) juu ya **Matumizi ya Misimu ya vijiweni katika lugha ya Kiswahili " Mifano katika jiji la Dar es Salaam"** uliangalia matumizi ya misimu ya vijiweni katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu uligundua kuwa kuna matumizi ya misimu ya vijiweni katika lugha Kiswahili. Vilevile umetuwezesha kujua kwa undani sababu za watu kutumia misimu ya vijiweni katika lugha hiyo. Hata hivyo utafiti huu haukujihusisha na misimu ya lugha ya Kiswahili inavyotumika katika mitandao ya kijamii. Hivyo, utafiti huu umeshawishika kuziba pengo hilo kwa kuangalia chimbuko la misimu katika mitandao ya kijamii.

Ngole, (2013) utafiti wake uliangalia **Lugha inayotumika katika masoko ya nguo za mitumba jijini Dar es Salaam.** Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba kuna aina ya lugha inayotumika katika masoko ya nguo za mitumba na lugha hiyo yaweza kuitwa lugha ya soko mitumba. Ngole katika utafiti wake tunaona haukujihusisha na masuala ya matumizi ya misimu ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii, hivyo utafiti huu utaziba pengo hilo**.**

Utafiti wa **Kipacha, (2014)** juu ya **misemo katika lugha za magari''** Ilionesha kwamba semi za magari ni mseto wa maandiko yenye uhuru zaidi, haufungwi

na kanuni za uandishi wa fasihi za kiafrika. Misemo iliyokusanywa na mtafiti ina hali ya usongombingo na mseto matini unaochanganya vidokezo, vifupisho, mafumbo, misemo ya mtaani,misimu, majina ya matukio, lakabu, kauli. Mtafiti amegundua kuwa utafiti huu vilevile haukuweza kujishughulisha na matumizi ya misimu ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii.

(i) Kiunga (2016) ameangalia maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususani facebook na Twitter. Utafiti wake uliangalia sifa za lugha inayotumika katika mitandao ya kijamii katika misingi ya kiisimu na kiisimu jamii.

Kutokana na pengo hilo utafiti huu uliona kuna haja ya kufanya utafiti ili kuziba hilo pengo.

(iii) **Matumizi ya Misimu katika muziki wa Hip hop** kwa kuangalia namna lugha ya kiswahili ilivyoharibiwa kutokana na matumizi ya misimu. Ally Almasi (2011) katika tasnifu yake iliyohusu ‘‘Mchango wa muziki wa Hip hop katika kukuza kiswahili’’. Omary(2009) amejadili matumizi ya misimu na kugawa misimu katika makundi sita kama ifuatavyo misimu inayohusu vilevi na starehe, misimu inayohusu mahusiano ya kimapenzi, misimu inayohusu jinsi (kike au kiume), misimu ya mavazi, misimu inayohusu hali ya kiuchumi na fedha na misimu inayohusu maumbile ya maumbo. Ameendelea kufafanua kuwa Ally amekwishatajwa kuwa wanamuziki wa Hip Hop hutumia misimu hii kwa kuzingatia maudhui ya kile wanachokizungumzia na kutokana na uteuzi wa misimu. Pia katika kazi hiyo ilieleza sababu za matumizi ya misimu katika muziki wa Hip Hop kigezo kikubwa kinachotumiwa katika kubeba dhana kuwa muziki wa Hip Hop unachangia.

(ii) **Lugha inayotumika katika masoko ya nguo za mitumba jijini Dar es Salaam** Costansia Ngole(2013) lengo la kazi yake kuchunguza upekee wa lugha inayotumika katika masoko ya nguo za mitumba jijini Dar es Salaam, matokeo ya utafiti huu yameonyesha kuwepo kwa lugha tofauti inayotumika katika masoko hayo ya mitumba jijini Dar es Salaam.

#### 2.2.1.3 Mapitio ya Kisera Juu ya Matumizi ya Misimu ya Lugha ya Kiswahili

Kivale (2013) alifanya utafiti kuhusu sera ya lugha ambao umeonesha udhaifu wa sera ya lugha ya Tanzania : Nini kifanyike. Utafiti huo umeonyesha udhaifu uliopo katika sera yetu ya lugha na ndio sababu kumekuwa na matumizi ya lugha ya misimu katika mitindo mbalimbali. Sera ya mamlaka ya mawasiliano juu ya matumizi ya lugha kwenye mitandao. Sheria za makosa ya kimtandao, (2015) imegusia mambo kumi ya kuzingatia ili makosa ya kimtandao yasimkute mtu na kumtia hatiani kati ya mambo hayo utafiti umeyaainisha mawili, jambo la kwanza:

(i) Epuka kusambaza au kutunga ujumbe unaoleta uchochezi wa kidini unaoweza kuvuruga amani na maelewano kwa jamii kupitia mitandao.

(ii) Epuka kushiriki kumchafua mtu, taasisi, kikundi cha watu kwanamna yoyote kupitia mitandao pia itakugharimu.

Kutokana na sheria hii watumiaji wa mitandao ya kijamii wamebuni mtindo wa lugha ambao utawaepusha na kuingia katika tuhuma za kushitakiwa na makosa ya kimtandao hivyo imewalazimu kutumia misimu ya lugha, na misemo mbalimbali ili kuweza kupunguza ukali wa maneno

### 2.2.2 Changamoto za Kutumia Misimu katika Mitandao ya Kijamii”

(i) Mapitio ya kinadharia

(ii) Mapitio ya kazi tangulizi

Utafiti wa Abdullah keshatajwa hapo juu utafiti huu umefafanua athari za kiisimu na zisizo za kiisimu zinazoletwa na lugha tandawazi. Mtafiti anaona watumiaji wa lugha ya Kiswahili wataelewa athari za lugha tandawazi katika Kiswahili na hivyo watakuwa makini na mtindo huu na mingine itakayoibuka katika jamii.

Katika utafiti wa Ally Almas (2011) keshatajwa katika kazi hiyo ilieleza sababu za matumizi ya misimu katika muziki wa Hip Hop kigezo kikubwa kinachotumiwa katika kubeba dhana kuwa muziki wa Hip Hop unachangia katika kuharibu lugha ya kiswahili ni kuwepo kwa matumizi ya misimu yaliyotamalaki kwenye nyimbo hizo.

### 2.2.3 Kiunzi cha Nadharia

TUKI, (2013) inaeleza kuwa nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza kutatua au kutekeleza jambo fulani. Wamitila, (2011) naye anaeleza kuwa nadharia ni mawazo, dhana au maelezo yanayotolewa kuelezea hali fulani, chanzo chake utendaji kazi wake na mwingiliano wake wa ndani na nje. Nadharia Jumuishi ya Giles ambayo hutambulisha nani anatumia lugha ipi uliasisiwa na kuendelezwa na Fishman (1972) Mkabala wa kinadharia uliotumika ni nani anatumia lugha ipi uliasisiwa na kuendelezwa na Fishman (1972) na baadae ulitumiwa na wataalamu wengine kama vile Parasher

(1980), Msanjila (1999) na Chacha (2001). Kimsingi mkabala huu wa kinadharia hutumika katika tafiti mbalimbali zinazohusu matumizi ya lugha yenye lengo la kutaka kujua nani, kwa maana kundi la jamii ipi linatumia lugha fulani au vipengele vya lugha fulani mara kwa mara katika mawasiliano ya kawaida ya jamii. Wanaisimu mbalimbali wamefasili dhana ya misimu kwa mujibu wa Msanjila na Wenzake, (2009) wanaeleza kuwa misimu ni aina ya misemo katika lugha ambayo huzuka na kutoweka. Sifa kuu ya misimu kwa mujibu wa Msanjila, (2009) misimu haidumu muda mrefu kwa kuwa ni lugha isiyo sanifu na watumiaji wa misimu huwa ni kikundi cha wazungumzaji wa lugha katika jamii ambao kimsingi huishi katika eneo moja.

Msanjila na wenzake,(2009) wanaendelea kueleza kuwa wazungumzaji wengi wa lugha hupenda kutumia lugha inayofahamika katika jamii yao kama njia mojawapo ya kuonyesha mshikamano, umoja na hata utambulisho wa namna fulani miongoni mwa kundi au tabaka la wazungumzaji wa kundi fulani. Kulingana na fasili ya Msanjila matumizi ya haya maneno ya misimu imekuwa ni changamoto miongoni mwa watumiaji wa misimu hiyo kwa sababu yanaleta ubaguzi kwa wale ambao hawaelewi maana ya maneno hayo ya misimu inayotumika katika mitandao ya kijamii. Miongoni mwa maneno hayo ni **kutumbuliwa, kumagufulisha, kujikitwanga, kihiyo likiwa na maana mtu asiye na vyeti sahihi vya kitaaluma** si watu wote wanaotumia mitandao ya kijamii wataelewa maana ya maneno hayo ya misimu.

Ngure,(2003) anaonekana kukubaliana na Msanjila kwa kiasi kikubwa isipokuwa yeye anaweka mkazo zaidi hasa pale anapodai kwamba uzukaji wa

misimu ni wa ghafla na wakati fulani hufuatana na mambo au matukio maalumu ya wakati au msimo huo, anaendelea kufafanua kuwa misimu huzuka/huibuka na kutoweka kufuatana na hali mbalimbali za kimazingira. Hata hivyo baadhi ya misimu hudumu na kuwa sehemu ya lugha.

Kulingana na fasili hizo zote juu zimeonesha pia namna misimu inavyozuka kutokana na hali au mabadiliko mbalimbali ya kijamii. Hivyo, miongoni mwa mabadiliko hayo ni maendeleo ya sayansi na teknolojia yalisababisha hata matumizi ya lugha yatumike kulingana na miktadha hiyo, hivyo katika kuwepo kwa maendeleo ya sayansi na tekinolojia mitandao ya kijamiii nayo imechukua sura mpya kwa kutumia misimu. Kulingana na tafiti ya N.Mohamed(2013)katika uatafiti wake nimeshaubainisha kwenye mwanzoni mwa sura hii umetumia nadharia kidhi ya mawasiliano, pia kazi ya Ali Haji (2016) katika kazi yake “maana za majina ya watu wa pemba katika lugha ya Kiswahili,uchunguzi kifani” katika kazi hii ametumia nadharia jumuishi.kazi zote mbili zimetumia nadharia za Giles, hivyo utafiti huu umetumia nadharia hizi mbili.Nadharia jumuishi ya utambulisho ya Giles (1979) inafanunua kwamba utambulisho wa mtu au jamii ni mchakato unaoendelea, ambao kimsingi unahusisha vibainishi vingi vinavyodumishwa na jamii ligha ambayo huunda kiini cha utambulisho wa jamii lugha hutumika katika jamii kama ishara ya kueleza utabulisho huo, jamii lugha inaundwa na wale watu wanaojiona na kujitambua wenyewe kuwa wao wanaotokana na jamii lugha nyingine hivyo kwa upande wa utafiti huu jamii lugha ni watumiaji wa mitandao ya kijamii na vibainishi ni maneno ya misimu na lugha hii ya misimu ipo tofauti na lugha nyingine. Nadharia kidhi ya mawasiliano (NKM) ya Giles(1973) ambayo ilijaribu kutafuta sababu za kuwepo kwa

mabadiliko ya wazunguaji katika mtindo wa matamshi na msamiati mipya wakati wa mawasiliano ya kijamii, NKM imesema kuwa binadamu hujitahidi kuzungumza lugha au kuiga namna Fulani ya matamshi ya lugha na msamiati mipya kutoka kwa sikilizaji wake ili tu aweze kukidhi haja ya mawasiliano. Katika utafiti huu maneno ya misimu ni msamiati mipya na yanatumika kwa minajili ya kukidhi awasiliano watumiaji wa mitandao ya kijamii hutumia msaiati mipya kukidhi haja yao ya kuwasiliana.

Makala katika gazeti la mwananchi la mwezi mei 19, 2013 lilieleza dhana ya mitandao ya kijamii kuwa ni tovuti ama mfumo maalumu unaowezesha watumiaji wake kuwasiliana na kutumiana taarifa kwa njia ya meseji, sauti na picha za mnato ama mtikisiko (video).

Baadhi ya mitandao hiyo ni kama “facebook”, “youtube” na “whatsap”. Pia utafiti utaangalia watumiaji wa lugha “sosholojia ya lugha”tofauti ndani ya lugha inaweza kuwa katika misingi ya kitabaka,kikazi, kijiografia au kibinafsi (Mekacha 2011:33) utofauti huo ndani ya lugha ndio kumesababisha kuzuka kwa misimu mbalimbali ambayo inatumika sana katika mitandao ya kijamii mfano **hapa kazi tu**, **figisufigisu, majipu,mariyoo** na mingine mingi. Utafiti utachunguza chanzo cha utokeaji wa maneno ya misimu kwa mujibu wa Masebo na mwenzake (2010) wanasema kuwa:

(i) Misimu huzuka kutokana na mabadiliko ya kihistoria yanayoikumba jamii katika nyakati mbalimbali. Misingi ya kuzuka misimu inakuwa ileile ya kutaka kuelezea dhana Fulani ambayo imejitokeza katika mfumo wa maisha ya wanajamii.

(ii) Misimu mingine huzuka kutokana na hali ya utani miongoni mwa watu mbalimbali mara nyingi misimu ya aina hii hubeba kebehi, dhihaka,kejeli, mabezo, dharau au kusifu kusiko kwa kawaida.

Utafiti utaangalia changamoto zinazotokana na matumizi ya misimu miongoni mwa walengwa wa utafiti na hususani katika mitandao ya kijamii. Kwa mujibu wa nadharia hii jumuishi ya utambulisho na nadharia kidhi ya mawasiliano Nadharia Kidhi ya Mawasiliano (NKM) inaona kuwa:

(i) Watu hueleza historia na uzoefu wao katika mawasiliano kupitia matamshi na tabia zao ili kuonesha kuwepo kwa ufanano wa matamshi na tabia fulani katika mazungumzo;

(ii) Mawasiliano huathiriwa na namna watu wanavyopokea na kutathmini nini kimetokea katika mazungumzo, yaani namna gani watu wanatafsiri na kuhukumu ujumbe uliobadilishwa katika mazungumzo; na


(iii) Mawasiliano hubadilika kulingana na kaida na hali ya kimuktadhainayofaa.

Utafiti ameamua kutumia nadharia hii kwa sababu ina uwezo wa kutumiwa katika maeneo yoyote ambayo yanahusisha mawasiliano; na utafiti huu pia unazungumzia. Dhana ya maeneo ya matumizi ya lugha imedhihirisha umuhimu usioepukika katika uchambuzi wa kiisimu jamii kwa mujibu wa (wolff katika Heine na Nurse 2000). Hii ni dhana inayohusu muktadha halisi wa kijamii na matumizi ya lugha katika jamii na katika utafiti huu umejikita katika matumizi ya maneno ya misimu yanavyotumika katika mitandao ya kijamii na kuchunguza changamoto za maneno hayo ya misimu miongonim mwa wazungumzaji vyuoni Morogoro . Dhana hii

inashabihiana na namna ya misimu ya lugha inavyotumika katika mitandao ya kijamii kwa kuzingatia mada ya mazungumzo, hivyo . Utafiti huu umeongozwa na maneno ya misimu kwa kuzingatia chanzo, kiasi cha matumizi na changamoto za kutumia maneno ya misimu hivyo matafiti akisukumwa na nadharia ya isimu jamii na namna lugha inavyotumika katika jamii mtafiti akaweza kubaini namna utumizi wa haya maneno ulivyochukua kasi katika mitandao ya kijamii.

**Jinsi Nadharia Ilivyotumika**

Nadharia hii imesaidia mtafiti kuchambua data na kuoanisha na matokeo ya utafiti kwani mtazamo wa watafitiwa kuhusiana na Chimbuko, kiasi cha matumizi na changamoto za kutumia maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii hivyo nadharia hii jumuishi ya Giles na nadharia kidhi ya mawasiliano imeweza kuakisi vibanishi lugha ambavyo ni maneno ya misimu pamoja na mitindo ya matamshi na msamiati mipya lengo la kuchunguza chanzo na sababu zake za utokeaji wa maneno ya misimu pia nadharia kidhi ya mawasiliano imejibu matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii, zimeweza kueleza vizuri mada ya utafiti huu . Mchoro ufuataо umeweza kueleza kwa kifupi malengo na mapendekezo ya utafiti huu kwa kuonyesha vigezo na malengo ya utafiti




**Kielelezo Na. 2.1: Nadharia ya Utafiti**

Chanzo: Imeigwa na kurekebishwa kutoka kwa Stufflebeam (1972)

## 2.3 Pengo la Utafiti

Licha ya utafiti wa Kiunga, M (2016) kuhusu maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususani facebook na twitter, utafiti uliweza kubaini kuwa uchovyanyaji msimbo, usilabishaji na sifa nyingine husaidia sana katika kuiga lugha ya mitandao ya kijamii. Upekee katika kutekeleza majukumu yake, vilevile utafiti uliangalia nafasi ya mafumbo au lugha ficho katika kuelewa anachomaanisha msemaji na ilibainika kuwa maana ya msamiati hutegemea muktadha wa usemi wenyewe. Hata hivyo utafiti huu pamoja na kazi zilizotangulia suala la matumizi ya misimu na

changamoto zake katika mitandao ya kijamii halijashughulikiwa kwa kiasi kikubwa. Aidha tafiti hizo hazijashughulikia kabisa suala la chimbuko na matumizi ya misimu ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Utafiti huu utashughulikia masuala hayo ambayo hayajashughulikiwa na kutoa mapendekezo juu ya namna ya kushughulikia changamoto hizo. Na pia utafiti huu utakuwa ni chachu ya tafiti nyingine zitakazofuatia ambazo zitashughulikia mada inayofanana na hii kwa utafiti zaidi.

# SURA YA TATU

# MBINU NA VIFAA VYA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Lengo kuu la sura hii ni kufafanua mbinu mbalimbali ambazo zimetumiaka katika mchakato wa kufanya utafiti hadi kufikia uchambuzi wa data zilizo kusanywa. Sura inaanza kwa kuelezea usanifu wa utafiti, eneo la utafiti na sababu za kuteua eneo hilo, usampulishaji kwa kuangalia aina ya walengwa waliotafitiwa. na jinsi mtafiti alivyo pata sampuli, mbinu mbalimbali zilizotumiwa na mtafiti katika kukusanya data. Aidha, maadili ya utafiti kwa kuangalia haki za mtafitiwa zimejadiliwa na mwisho inaeleza kwa ufupi jinsi data zilivyochambuliwa, majadiliano na matokeo ya majadilianona mwisho inatoa muhtasari wa sura nzima zana za utafiti na vifaa ambayo vimetumika katika utafiti huu hadi kufikia uchambuzi wa data.

## 3.2 Sampuli na Usampulishaji

### 3.2.1 Sampuli ya Watafitiwa

Mligo (2012) anaeleza kuwa sampuli ni kundi fulani la watu lililoko ndani ya mkusanyiko wa watu ambao mtafiti anaamini kwamba linazo habari ambazo mtafiti anaamini zinamwezesha kujibu swali lake la utafiti, pia Cohen na Manion (2003) wamefafanua sampuli ni sehemu ndogo ya kundi kubwa na Creswell (2005) wameeleza kuwa sampuli ni sehemu ya kundi lengwa ambalo mtafiti anapanga kulisoma kwa ajili ya kujumuisha kuhusu kundi lengwa Kundi lengwa ni jumla ya watu wote ambao huhusishwa katika utafiti (Kothari 2004; Bryman; 2004, Komba na Tromp, 2006).

Kuchagua sampuli ni kuchagua kundi dogo la watu katika mkusanyiko wenye makundi ya aina nyingi kwa malengo maalumu aliyonayo mtafiti kwa ajili ya utafiti wake. Kwa kuwa si rahisi kwa mtafiti kuwatafiti watu wengi katika eneo kubwa. Hivyo utafiti huu umelenga sampuli ya watu wachache ambayo imesaidia kujibu maswali yaliyolengwa kwenye utafiti ili huu kupata data.Cooper (1989) na Vans (1990) wanasema kuwa kundi lengwa ni wanachama wote, mtu mmoja, kikundi cha watu ambao mtafiti amekusudia kuhusisha katika utafiti wake. Hivyo, utafiti huu umechagua sampuli kutoka vyuo vitatu ambavyo ni Chuo cha Ualimu Morogoro, Chuo cha Ualimu Muhonda, Chuo kikuu cha Kiisilamu (MUMU), kati ya vyuo sita vya Mjini Morogoro ambavyo vimeweza kumsaidia mtafiti kupata data sahihi za utafiti wake. Kila Chuo kimetoa idadi ya wanachuo 20, wahadhiri na wakufunzi 10. Aidha Sampuli ya utafiti huu ni ya watafitiwa wote wanachuo na wakufunzi, ambapo kwa mujibu wa Kothari(2012), kiasi hicho cha Sampuli kimetosha kuwakilisha kundi zima la watafitiwa.

### 3.2.2 Mbinu ya Usampulishaji

Sigh (2007), usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Kwa mujibu Komb K.D na Tromp L.D (2006) muundo wa usampulishaji ni sehemu ya mpango wa utafiti ambao unaonesha jambo ambalo limechaguliwakwa uchunguzi. Zipo mbinu mbili za usampulishaji,.usampulishaji wa nasibu na usampulishaji linganishi katika utafiti huu usampulishaji nasibu ndio uliotumika. Ruane (2005), anafafanua kuwa usampulishaji .nasibu kuwa ni mchakato wa kuchagua sampuli ambapo uwezakano

wa kuchagua mtu yeyote katika kundi lengwa huwa mkubwa. Koul, (2009) anafafanua kuwa usampulishaji nasibu ni njia rahisi ya usampulishaji na kila kitu katika vitu au vikundi hupewa nafasi sawa ya kuchaguliwa. Anaendelea kusema kwamba usampulishaji nasibu linganishi ni usampulishaji unaoweza kutumiwa pale unapowagawa watafitiwa kwa kugawa watu kwa uwiano sawa. Hivyo utafiti huu umetumia mbinu ya usampulishaji nasibu ambayo mtafiti amehusika kufanya utafiti katika vyuo vitatu kati ya vyuo saba ambavyo vilipatikana kwa njia ya bahati nasibu, kwa njia ya bahati nasibu wamechaguliwa wakufunzi 16, kati yao kuna wanaume 9 na wanawake 7, na wahadhiri wanne ambao wamegawanyika kuwa wanaume 2 na wanawake 2. Makundi haya yamepatikana kutoka katika kila kundi la wahadhiri na wakufunzi wanaofundisha kozi za masomo ya lugha tu. Aidha wamechaguliwa wanachuo wa kike na wakiume kwa idadi sawa yaani wanaume 40 na wanawake 40 na kufanya jumla ya sampuli ya wanachuo kufikia theanini. Makundi ya watafitiwa na idadi yao imeoneshwa katika utafiti huu umefanyika katika vyuo vitatu vya Ualimu ambavyo ni Chuo cha Ualimu Morogoro, Chuo cha Ualimu Muhonda na Chuo kikuu Cha Kiislamu Morogoro mtafiti amechagua vyuo hivi kwa sababu zifuatazo Chuo cha Ualimu Morogoro kwa kuwa ni Chuo cha muda mrefu na pia ni kimekuwa rahisi kwa mtafiti kupata data. Vilevile, uchaguzi wa Chuo cha Ualimu Muhonda umefanyika kwa kuwa ni Chuo cha Ualimu ambacho kinatoa ngazi ya cheti na kina wanafunzi wanaosoma somo la Kiswahili. Mwisho ni Chuo kikuu cha Kiislamu Morogoro ambacho mtafiti ameona ni chuo kikuu pekee ambacho kina wanafunzi wanaosoma somo la kiswahili na kina wahadhiri wanaofundisha lugha ya Kiswahili miongoni mwa vyuo vikuu vingine vinavyopatikana mkoani

Morogoro.Hivyo, uteuzi wa vyuo vyote vitatu umefanyika vizuri kwa kuwa unatutanabaisha kuwa lugha ya Kiswahili ndio lugha ya kufundishia, hivyo kuwa rahisi kwa utafiti kupata data kamili.

Utafiti huu umehusisha sampuli ya watafitiwa mia moja ( 100) katika mchanganuo ufuatao wanachuo ni themanini, wakufunzi kumi na sita 16 na wahadhiri ni wanne 4 watafitiwa hawa wanasifa tofauti kwa vigezo vya umri, uelewa na ubobevu wa kufundisha lugha ya Kiswahili.

**Mchakato wa Usampulishaji**

**Jedwali Na. 3.1: Sampuli ya Watafitiwa**

| SAMPULI | WANAUME | WANAWAKE | JUMLA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Wanachuo | 40 | 40 | 80 | 80 |
| Wakufunzi | 8 | 8 | 16 | 16 |
| Wahadhiri | 2 | 2 | 4 | 4 |
| **Jumla** | **50** | **50** | **100** | **100** |

Chanzo: Utafiti 2017

Mtafiti alifanya Majadiliano na wahadhiri wanne (4) kutoka sampuli ya chuo A ambacho ni Chuo kikuu cha Kiislamu Morogoro, wakufunzi sita (6) kutoka sampuli ya chuo B ambacho ni chuo cha Ualimu Muhonda na wakufunzi kumi (10) kutoka sampuli ya Chuo C ambacho ni chuo cha Ualimu Morogoro. Watafitiwa hao walitoka katika jinsia tofauti kama inavyojionesha katika jedwali ambalo limeonyesha watafitiwa wanachuo kwa jinsi zao

**Jedwali Na. 3.2: Sampuli ya Watafitiwa Wanachuo kwa Kila Chuo**

| SAMPULI | CHUO A | CHUO B | CHUO C | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| WANAUME | 10 | 15 | 15 | 40 |
| WANAWAKE | 12 | 15 | 13 | 40 |
| **JUMLA** | **22** | **30** | **28** | **80** |

Chanzo: Utafiti 2017

## 3.3 Mbinu za Kuchanganua Data Muundo/ Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu ulitumia ainambili za mikabala katika uchanganuzi wa data. Kothari (1993) anafafanua kuwa zipo aina kuumbili za mikabala ya utafiti, mikabala hiyo ni: mkabala wa maelezo na mkabala wa kiidadi wakati ambapo mkabala wa maelezo inahusika na tathmini isiyo bayana ya mielekeo, maoni na mienendo (Punch,2004). Mkabala wa kiidadi inamaanisha uchunguzi bayana wa kisayansi wa masuala ya kijamii kupitia mbinu za ukokotoaji wa takwimu, hisabati/ tarakimu (Kahn, 2011). Aidha, Kothari(1993) anadai kwamba, wakati utafiti wa kiidadi imejikita katika msingi wa vipimo vya idadi au kiasi na kutumika katika masuala yanayoweza kueleza kwa idadi. Utafiti wa maelezo unajihusisha zaidi na upimaji kwa maelezo ya masuala ya jamii yanayotathiminiwa kwa ubora au aina ya masuala hayo. Katika utafiti huu mkabala utakaotumika ni wa kimaelezo na wa idadi kwa wakati mmoja( mkabala mchanganyiko).

## 3.4 Mbinu na Njia za Kukusanya Data

Data kama anavyotueleza Adam (2008) ni vielelezo vinavyokubalika ambavyo vinathibitisha ukweli wa matokeo. Data za msingi (awali) kama anavyozieleza Kothari (2004) ni zile data ambazo hukusanywa kwa mara ya kwanza. Data hizi

zilikusanywa wakati mtafiti yuko uwandani, katika sehemu zilizoteuliwa.Data hizi zilijibu maswali ya utafiti. Data hizi zilinukuliwa kwenye madaftari; na kinasa sauti kilitumika kwa ajili ya kurekodi taarifa. Data za awali huaminiwa sana kwa sababu hukusanywa moja kwa moja kutoka kwenye tukio, mtafiti ametumia data za awali kwa kuwa zimemsaidia kupata majibu sahihi kutokana na mada yake ya utafiti ambayo inahitaji majibu sahihi kutoka uwandani zaidi.

Data za upili ni zile ambazo tayari zilizokusanywa na zimeshatumika na zimehifadhiwa (Kothari: Amekwisahtajwa). Aina ya data zilizotumika katika utafiti huu ni data za msingi na za upili.“ Njia zitakazotumika kukusanyia data ni kusoma ujumbe mfupi wa aina mbalimbali unaotumwa kupitia mitandao ya kijamii. Njia hii imetumika katika ukusanyaji wa dataza awali. Lengo ni kupata hayo maneno ya misimu yanayotumika.Pia katika kupitia ujumbe mbalimbali unaotumwa kwenye mitandao ya kijamii. Mfano wa ujumbe kama huu kupitia ‘whatsaap’ (hata kama kuna **mchepuko** unanyemelea mtu anautaja na kuomba msamaha huku hajaulizwa 24/julai 2016 saa 23:18).

Ujumbe mwingine: “habari za jpili wadau naomba msaada wenu hapa kwetu vijana wote waliokuwa wameomba kujiunga na kozi mbalimbali kupitiaNACTE hawajachaguliwa kisa kontena la UDOM naomba uzoefu kwa Wenzangu mliopewa **kontena** kama sisi maana sijui watoto wa watu wanapiga simu mpaka basi” “bahati mbaya **vicheche** wamepitiwa seminari” “mimi **jipu”.**Data hizi pia mtafiti amezipata kupitia maandiko ya wataalamu mbalimbali pamoja na ripoti za aina tofauti. Taarifa hizi pia zitakusanywa kwa kuangalia kazi zilizopita kuhusiana na mada kwa kuangalia vitabu, majarida, na mashapisho mbalimbali**.**

### 3.4.1 Mbinu ya Hojaji

Kwa mujibu wa Kothari (keshatajwa), hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambayo mtafiti huandika maswali na baadaye huwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia. Kwa mujibu Kothari (2004) hojaji ni mbinu ya kukusanyia data ambayo mtafiti huandika maswali na baadae kuwapa watoa taarifa ili wayajibu na kumrudishia. Mtafiti alitumia mbinu hii na ilimsaidia kupata data kwa urahisi na haraka zaidi.

Pia Walliman (2011) anaeleza kuwa kuna maswali ya hojaji ya aina mbili. Aina ya kwanza, ni maswali fungeambayo hutoa fursa kwa watafitiwa kuchagua jawabu. Aina hii ni rahisi kujibu na kuchanganua. Pia, inasaidia kupata majibu mahususi na huepusha upendeleo. Aina ya pili ya maswali ya hojaji ni yasiyo funge, ambayo hutoa fursa au uhuru kwa watafitiwa kueleza wanachokijua pia husaidi kupata taarifa nyingi zaidi.

Mbinu ya hojaji iliyotumika katika utafiti huu imejumuisha aina zote mbili za maswali yanayokuwemo katika hojaji, yaani maswali funge na maswali yasiyo funge. Mtafiti aliamua kuchanganya aina zote za maswali ili kuepuka mapungufu yanayoweza kutokea katika mbinu hizi mbili, ikizingatiwa kuwa kila moja ina mapungufu yake. Hivyo, mbinu hizo zikitumika kwa pamoja kila moja husaidia kuziba mapungufu ya nyenzie. Mtafiti aliwapa watafitiwa wanachuo hojaji wajaze papo kwa papo na ilikuwa rahisi kupata data ambazo zimesaidia katika utafiti wake.

### 3.4.2 Mbinu ya Usaili

Babbie (1992)anasema usaili ni mbinu inayohusisha mawasiliano ya moja kwa moja baina ya mtafiti na wahojiwa na mtafiti hupata maelezo zaidi kuhusu

baadhi ya mambo ya ambayo yasingewekwa bayana kupitia mbinu nyingine ya utafiti.

Kombo na Tromp (2006)wanasema mahojiano ni majibizano ya ana kwa ana au ya simu kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani Mtafiti atafanya majadiliano ya ana kwa ana na watafitiwa kwa lengo la kupata data ambazo zitasaidia kubaini sababu za kuibuka kwa hayo maneno ya misimu na mchango wake miongoni mwa watafitiwa wanapowasiliana katika mitandao ya kijamii. Katika usaili huu mtafitiwa ametumia hojaji. Mtafiti aliweza kufanya majadiliano kwa njia ya simu na wahadhiri wawili alioshindwa kukutana nao alivyokwenda kufanya majadiliano ya kwa pamoja alivyokwenda chuoni, mtafiti aliweza hata kuuliza maswali nje ya maswali ya majadiliano ambayo mtafiti yalimsaidia kujibu mada ya utafiti.

### 3.4.3 Mbinu ya Ushuhudiaji

Kothari (1990) **U**shuhudiaji ni mbinu ambayo taarifa hukusanywa na mtafiti mwenyewe kwa kuchunguza tabia za watafitiwa wake bila ya kuwauliza maswali yoyote watafitiwa, Hapa mtafiti hutathimini moja kwa moja kupitia watafitiwa wake. pia mbinu ya uchunguzi ni njia ya kukusanya taarifa kwa kuangalia tabia ambazo zimezoeleka au mchakato wenye mahusiano,matukio au kuchukua tabia zinazoonekana katika mazingira ya uhalisia (Drury,1992).

Uchunguzi hutoa taarifa iliyowazi kwa mtafiti mawasiliano yao katika mitandao ya kijamii kwa kuwa ni miongoni mwa watumiaji hivyo mtafiti ataweza kubaini ni maneno gani ya misimu wanayoyatumia zaidi na sababu zinazochangia

watumiaji wa mitandao ya kijamii kutumia zaidi misimu. Vilevile mtafiti ataweza kubaini ni kwa kiasi gani maneno ya misimu yamesaidia kurahisisha mawasiliano miongoni mwa watumiaji wa mitandao ya kijamii na katika ushuhudiaji mtafiti aebaini changamoto zinazotokana na matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii. Pia aliweza kupakua picha ambazo amezidukua kutoka katika mitandao ya kijamii. Mbinu hii imetumika katika utafiti huu kwa kuwa mtafiti nae ni mkufunzi na pia alikuwa ni sehemu ya majadiliano yake kuligana na maswali ya majadiliano katika kiambatisho Na 04.

## 3.5 Mbinu ya Kupitia Maandiko Mbalimbali

Kothari (2004).anaeleza kuwa mbinu ya kupitia maandiko mbalimbali ni njia mojawapo ya data za upili .katika ukusanyaji wa taarifa ambayo husaidia kutoa data za upili(Kwa kupitia na kusoma ripoti mbalimbali na tasnifu zilizotangulia kwa ajili ya mtafiti kupata taarifa zaidi kuhusiana na mada yake yautafiti ‘‘ripoti ya makosa ya kimtandao’’ (2010 ) Nunuu Abdallah (2013)**“ matumizi ya simu ya kiganjani”** Moche Kihombo (2013) ‘‘Matumizi ya mtindo wa mawasiliano yasiyo rasmi kwa lugha ya kiswahili katika redio’’ utafiti wa Timothy. K (2016) “**maana ya usemi na mazungumzo katika mitandao ya kijamii hususani facebook na Twitter”**.licha ya mtafiti kupitia maandiko mbalimbali pia mtafiti aliweza kupitia ujumbe mbalimbali kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya jumbe hizo nimeziainisha katika sura ya nne.

## 3.5 Uhalali na Uimara wa Zana za Utafiti

Kwa mujibu wa Best na Khan wameshatajwa wanafafanua uhalali wa zana za utafiti ni uthaminishaji wa ukusanyaji wa taarifa na utaratibu ambao unaruhusu

kupima kilichokusudiwa kupimwa. Uimara/ uhalisia wa zana za utafiti ni kuweza kuonyesha kiwango cha juu cha vifaa vya utafiti ambavyo vitaleta matokeo mazuri. Mtafiti amechagua zana za utafiti ambazo zilipimika na kumsaidia kupata taarifa aliyoikusudia ametumiahojaji, majadiliano, uchunguzi/ ushuhudiaji, orodha hakiki ya manemo ya misimu na maana yake au utumikaji wake katika mitandao ya kijamii.

Hojaji iliweza kuuliza maswali yote yanayojibu maswali ya utafiti na malengo yake na orodha hakiki majibu yake yaliweza kupimika na maswali ya majadiliano aliyoyatumia kwa wakufunzi na wahadhiri yaliweza kuibua mjadala chanya ambao umemsaidia mtafiti kupata taarifa aliyokusudia.

## 3.6 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni muhimu katika mchakato mzima wa utafiti. Katika kuonesha umuhimu wa vifaa na wakati wa matumizi katika utafiti kwa kuangalia aina ya vifaa vinavyoendana na kipindi hiki cha sayansi na teknolojia Mulokozi (1983) ameweza amefafanua kuwa vifaa vya utafiti vinavyotumika siku hizi ni kama kalamu na karatasi, tepurekoda, tepuvideo, kamera, kamera ya sinema, na transleta (mashine zinazotafsiri maandishi kwa msaada wa kompyuta). Utafiti huu umetumia vifaa kalamu, karatasi,simu ya mkononi shajara na kompyuta. Mtafiti alivitumia vifaa hivi wakati wote, kuanzia mwanzo hadi kukamilika kwa utafiti kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na kukamilisha mchakato mzima wa utafiti.

### 3.6.1 Shajala na Kalamu

Shajara na kalamu vilichukua nafasi kubwa katika utafiti huu ili kuandika maneno ya misimu yaliyokuwa yanazuka kila siku wakati wa utafiti. Vifaa hivyo vilitumika ili

kuandikia na kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya kila siku huku zikionesha siku, tarehe, muda na mahali yalipofanyika mahojiano kati ya mtafiti na mtafitiwa. Mtafiti alitumia vifaa hivyo kwa kuwa havina gharama na ni rahisi katika ubebaji wake. Licha ya faida ya vifaa hivi kwa upande mwingine ni hasara kwani vikimwagikiwa na maji kwa bahati mbaya maandishi huweza kufutika.

### 3.6.2 Kompyuta/Ngamizi/Tarakilishi

Kompyuta ni chombo cha kielektoniki chenye uwezo wa kupokea na kukusanya taarifa (data) halafu kuzishughulikia. Kifaa hiki kilitumika katika utafiti huu katika kutafuta matini za kielektroniki zote zilizohusiana na mada tafitiwa na kuzihifadhi. Kompyuta ilisaidia utafiti huu kuwa na kumbukumbu ya kudumu kwa ajili ya vizazi vijavyo. Hata hivyo, kukatika kwa umeme, tatizo la mtandao kulingana na maeneo, kuharibika kwa kompyuta ilikuwa ni changamoto katika kukamilisha utafiti kwa wakati.

### 3.6.3 Simu ya Mkononi

Simu ya mkononi ni kifaa ambacho kilitumika katika kupokea na kukusanya data. Utafiti ulitumia kifaa hiki katika kutafuta matini za kielekroniki zote zinazohusiana na mada husika. Pia ilisaidia kukusanya na kuhifadhi data kwa ajili ya kumbukumbu za kizazi kijacho na kuzihifadhi kwenye barua pepe. Hata hivyo kukatika kwa umeme na kutokuwa na kifaa cha kuhifadhi umeme (power bank) pale tatizo la kukatika kwa umeme linapotokea na simu kuishiwa umeme. Kukosekana kwa mtandao wa uhakika kwa sababu kuna wakati kulikuwa kunakukatika kwa mawasiliano.

### 3.7 Changamoto Wakati wa Kukusanya Data

Pamoja na kuwa utafiti huu umekamilika, mtafiti alikutana na changamoto kadhaa ambazo kama zinavyojionesha: kwanza ugumu wa kuwapata watafitiwa kwani muda wa kukusanya data vyuo vingi vilikuwa kwenye likizo mpaka ilimlazimu mtafiti kubadilisha chuo kimoja ambacho alishindwa kabisa kuwapata wanachuo na wahadhiri. Mfano katika Chuo Kikuu Cha Kiislamu Morogoro mtafiti alishindwa kabisa kukutana na wahadhiri wa Chuo hicho kwa ajili ya majadiliano ya pamoja kama alivyofanya kwa vyuo viwili vya ualimu Mhonda na Chuo cha Ualimu Morogoro.

Mtafiti alifanya hivyo kutokana na wahadhiri hao ambao ni wanne tu wanaofundisha somo la Kiswahili Chuoni hapo kuwa nje ya ofisi kutokana na likizo na kuwa na majukumu mengine kikazi. Hivyo, mtafiti ili mlazimu kufanya mahojiano na wahadhiri hao kwa njia ya simu huku akiwauliza yale yale maswali yaliyohitaji majadiliano na hapa ilimlazimu mtafiti kuzungumza na wataalamu hao mmoja mmoja.

### 3.8 Maadili katika Uandishi wa Ripoti

Mligo (2012) anaeleza maadili ni kanuni zilizowekwa na kukubaliwa na jamii ili zitumike kuongoza mwenendo wa maisha na tabia halisi ya maisha ya wanajamii husika aidha, Aeker (2002) kama alivyonukuliwa na Adam (2008) anataja maadili ya utafiti kuwa ni pamoja na haki ya mtafitiwa kuhakikishiwa usalama wake, halikadhalika maadili ya utafiti ni kuepuka wizi wa maneno, mawazo au vifungu vya maneno kutoka kwa mtafiti mwenyewe au watu wengine Mligo ( 2012).

Pia mtafiti anatakiwa pia kutunza siri za watafitiwa wake pale ambapo amefanya nao mahojiano. Hata hivyo, mtafiti amejitahidi kutunza siri na malezo au mahojiano yoyote aliyoyafanya na watafitiwa, hivyo yataendelea kuwa siri baina yake na watafitiwa na mwandishi wa ripoti hii amezingatia hilo kwani hata katika hojaji yake alibainisha kuwa chochote mtafitiwa atakachokieleza kitakuwa siri katika kukamilisha tasnifu yake.

Hivyo mtafiti atalazimika kutunza siri kwa kuheshimu maadili ya utafiti itapobidi. haki ya kujua madhumuni ya utafiti, haki ya kupata matokeo ya utafiti,haki ya kujibu maswali na kukataa wakati wa kushiriki kwenye utafiti. Mtafiti ametambua haki zote hizi na amezitekeleza. Kwa kuwa utafiti huu una madhumuni ya taaluma tu na si vinginevyo, maadili yamezingatiwa na wala mtafiti hatotoa siri za mtafitiwa kwa kuandika jina na kile alichochangia kwa kusema au kuandika. Maadili ya utafiti, ukusanyaji na uchambuzi wa data pia yameelezwa kwa ufupi.

## 3.9 Hitimisho

Sura hii imefafanua mbinu na njia mbalimbali ambazo utafiti umetumia katika kukusanya data na jinsi zilivyotumika ili kuwa na data kamili. Sura inayofuata itafafanua kwa undani uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka uwandani na maktaba.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHANGANUZI WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kuwasilisha na kuchambua data zilizokusanywa juu ya "Matumizi ya Misimu katika mitandao ya kijamii na changamoto zake kwa wazungumzaji wa lugha ya kiswahili." Data zote zilizokusanywa kwa njia ya hojaji, mahojiano, uchunguzi na usaili zinawasilishwa na kuchambuliwa kwa kina katika sura hii. Data za msingi zimetumika katika utafiti huu. Vertanian (2011) anaeleza kuwa data za msingi ni data ambazo zimekusanywa na mtafiti kwa kutumia mbinu kama hojaji, mahojiano, vikundi lengwa, uchunguzi au mbinu nyingine. Data hizi hutoka moja kwa moja kwa watafitiwa. Aidha, utafiti huu umetumia data za aina mbili. Aina ya kwanza ni data za ujumbe katika mitandao ya kijamii na aina ya pili ni data zinazotokana na mawazo na maoni ya watafitiwa kuhusu matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii. Data zilizopatikana kutoka kwa watafitiwa zimegawanywa na kuchambuliwa kwa kufuata aina nne za sampuli ambazo ni A, B, C na D. Sampuli A ni wanachuo wa Chuo kikuu cha kiislamu Morogoro. Sampuli B ni wanachuo wa Chuo Cha Ualimu Muhonda na sampuli C ni wanachuo wa Chuo Cha Ualimu Morogoro. Sampuli A ni kiwakilishi cha Chuo Kikuu Cha Kiislamu Morogoro. Mgawanyo huu umefanyika ili kutoa fursa kwa mtafiti kuchanganua data kwa urahisi na kufanya ulinganishi wa matokeo ya watafitiwa. Sura inaanza kwa kuwasilisha data na kumalizia na uchambuzi wa data. Uwasilishaji na uchambuzi huo wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti na maswali yanayoambatana na malengo hayo. Maswali hayo yamelenga maeneo yafuatayo:

(i) Kuchambua chanzo cha utokeaji wa maneno ya misimu kwenye mitandao ya kijamii.

(ii) Kuchambua kiasi cha utumiaji wa maneno ya misimu miongoni mwa wanachuo katika mitandao ya kijamii na;

(iii) Kuchunguza changamoto za kutumia misimu ya lugha ya Kiswahili katika mawasiliano kwenye mitandao ya kijamii.

## 4.2 Chanzo na Sababu za Utokeaji wa Maneno ya Misimu kwenye Mitandao ya Kijamii

Chanzo cha misimu kama ilivyoelezwa katika sura ya kwanza kulingana na miongoni mwa wataalamu kama Nyambari na Masebo (2002) na Ngure (2003) imeonesha kuwa chanzo cha maneno ya misimu ni mabadiliko ya kihistoria yanayoikumba jamii katika nyanja mbalimbali. Nyanja hizo ni kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ambapo maneno mbalimbali huibuka ili kuelezea hisia za wazungumzaji katika muktadha uliopo.

Utafiti uliofanyika katika vyuo vya ualimu Morogoro ambao ulihitaji kuchanganua matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii na changamoto zake kwa wazungumzaji. Utafiti huo kulingana na kundi lengwa uliweza kubaini chanzo cha utokeaji wa maneno ya misimu kupitia majadiliano yaliyofanyika vyuoni hapo. Watafitiwa walibaini kuwa maneno ya misimu huibuka katika jamii kutokana na mabadiliko ya kihistoria ambayo hutokea kwa upande wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mabadiliko ya kisiasa yaliweza kuibuka na maneno mbalimabali miongoni mwake ni kama yanavyojitokeza katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 4.1: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kisiasa**

| **ORODHA YA MANENO YA MISIMU** |
|---|
| Kutumbua majipu |
| Mwendokasi |
| Ukawa |

Chanzo: Misimu ya Wanachuo, 2017

Kwa upande wa kiuchumi, watafitiwa waliweza kuorodhesha baadhi ya maneno ya misimu ambayo yameibuka sana katika mitandao ya kijamii. Miongoni mwa maneno yaliyoibuka kulingana na nyanja hiyo ni kama yanavyojjitokeza katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 4.2: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kiuchumi**

| **ORODHA YA MANENO YA MISIMU** |
|---|
| Kuchakachua |
| Hapa kazi tu |

Chanzo: Misimu ya Wanachuo, 2017

Mwisho kwa upande wa kijamii, utafiti ulibaini kuwa maneno ya misimu yaliyoibuka katika nyanja hii yalibeba kiasi kikubwa cha maneno yaliyopatikana katika orodha hakiki ambayo mtafiti aliitumia kukusanya maneno ya misimu miongoni mwa wanachuo husika. Miongoni mwa maneno hayo yameweza kujitokeza kama jedwali lifuatalo linavyoonesha.

**Jedwali Na. 4.3: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kijamii**

| **ORODHA YA MANENO YA MISIMU** |
| --- |
| Kutafuta kiki |
| kuperuzi |
| muziki wa kizazi kipya |
| mademu |
| dada poa |
| Mrupo |
| kibendi |
| Zombi |
| Zege |
| Kuzingua |
| Kilaza |

Chanzo: Misimu ya Wanachuo, 2017

Mabadiliko ya kijamii pia kupitia matukio tofauti yanayojitokeza miongoni mwa wanachuo yamekuwa ni chachu ya kuibuka maneno ya misimu. Mfano katika picha ambayo mtafiti aliweza kuipata kupitia watafitiwa inaonesha baadhi ya maneno yametokana na wanajamii wenyewe kuyaibua kutokana na matukio tofauti kama burudani, utani n.k. Neno lililoibuka kipindi cha miaka ya 1970 ni kilaza. Pia, neno hili lilipata umaarufu tena baada ya Rais Magufuli kuwaita 'vilaza' wanafunzi elfu saba mia nane na mbili (7802) waliokuwa wakichukua kozi ya diploma chuo kikuu cha Dodoma ambao walifukuzwa na Rais na kuwataka wakatafute vyuo vinavyowafaa vya 'ukilaza'. Picha inayofuata ilipakuliwa kuonesha chimbuko la neno la msimu wa

‘kilaza’ kutokana na matukio ya burudani na utani enzi za mwanamuziki Mbaraka Mwinshehe.

Neno la msimu ‘kilaza’ kulingana na majibu ya watafitiwa waliweza kubaini ujumbe ambao ulikuwa unaeleza chanzo cha neno la msimu kilaza Kulingana na picha hiyo hapo chini inaonesha kuwa kutokuwa na uwezo mkubwa katika kufanya jambo inaweza kuwa la kitaaluma au mashindano tofautitofauti kwa mfano katika picha hiyo hapo chini msimu wa kilaza ulitokana na mwanamziki Juma Kilaza kusindwa kupiga gitaa kumshinda Mbaraka Mwinshehe, kutokana na alivyosema uliibua msimu wa kilaza kwa wanafunzi au watu ukiwa na maana ya uwezo mdogo wa kufanyajambo




**Kielelezo 4.1: Dhana ya Msimu Kilaza**

Chanzo: majbu ya watafitiwa kutokana na  Mitandao ya kijamii 2017)

Majibu ya sampuli hii ya watafitiwa yalijitokeza kwa maana tofauti miongoni mwao katika utafiti huu. Hata hivyo, majibu hayo yalidhihirisha kuwa misimu ni maneno yanayozuka pasipokuwa na makubaliano baina ya watu na hutumiwa miongoni mwa watu ambao huweza kuelewana wao wenyewe. Vilevile, maneno ya misimu hiyo hutumika katika muktadha maalamu kutokana na matukio na nyakati tofauti. Hata hivyo, utafiti unaonesha kuwa mara nyingine maneno ya misimu huweza kudumu kwa muda mrefu ama kupotea baada ya hayo matukio/nyakati kupita.

Hivyo, chimbuko la maneno ya misimu hutokana na matukio mbalimbali yanayotokea katika jamii. Matukio hayo yaweza kuwa ya huzuni au furaha kutokana na vipindi mbalimbali vya kihistoria. Licha ya sampuli hii kueleza sababu zilizopelekea chanzo cha misimu miongoni mwa watafitiwa walifafanua maana ya mitandao ya kijamii. Kwa kuwa lilikuwa ni moja ya swali la majadiliano ambalo liliwawezesha watafitiwa kujibu vema malengo ya utafiti Watafitiwa walifafanua kuwa mitandao ya kijamii ni njia za mawasiliano kupitia simu na kompyuta ambapo watu huweza kutumiana jumbe mbalimbali za maandishi, nyimbo, video nakadhalika. Hata hivyo watafitiwa walitoa maneno ya misimu na maana zake kama ifuatavyo: Jedwali linaonesha misimu iliyotokana na matukio mbalimbali.

**Jedwali Na. 4.4: Orodha ya Maneno ya Misimu Kutokana na Matukio**

| **Orodha ya Maneno ya Misimu** | **Maana/Matumizi Yake** |
|---|---|
| Jipu/ Majipu | Kuonesha watu wasio na sifa stahiki katika shughuli au maeneo fulani. Au kutokufaa katika utendaji wa kazi katika uongozi. |
| Hewa | Watu wasiokuwepo lakini wako kwenye orodha ya wanafunzi au watumishi wa serikali ili kupata huduma kama fedha nakadhalika. |
| Hapa kazi tu | Hali ya kufanya kazi kwa kila mwana jamii |
| Kilaza | Uwezo mdogo wa kufanya jambo |

Chanzo: Uwandani 2017

**Tafsiri ya Matokeo**

Kutokana na majadiliano kati ya mtafiti na watafitiwa, utafiti uliweza kubaini kuwa chimbuko la misimu ni kuzuka kwa maneno maalum ambayo huibuka katika muktadha maalum. Pia misimu huweza kuzuka kutokana na matukio mbalimbali yanayojitokeza katika jamii ambayo yanaweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Majadilianao yaliyofanyika yaliweza kubainisha baadhi ya misimu ambayo inatumika katika mazingira tofauti kulingana na kipindi hiki cha mabadiliko ya kihistoria. Katika kipindi cha awamu ya tano ya uongozi wa Raisi John Joseph Pombe Magufuli, Mheshimiwa Rais aliweza kukemea suala la watumishi wa serikali wasiojulikanana mahali popote ila wako katika orodha ya mishahara na marupurupu mengine ya serikali. Hotuba ya kwanza ya Mheshimiwa Rais J. P Magufuli bungeni mara baada ya kutangazwa kuwa Rais wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais alifafanua mipango mbalimbali katika serikali yake ya awamu ya tano na jinsi atakavyofanya kazi tofauti na viongozi kutoka katika awamu zilizopita. Rais alitangaza kuwa atashughulikia kikamilifu suala la matumizi mabovu ya fedha kwa watumishi wake, na kukata mianya yote ambayo inafanya kuwe na matumizi mabovu ya fedha. Aliendelea kusema kuwa atapunguza au kuondoa kabisa matumizi ya fedha kwenye safari za viongozi ndani na nje ya nchi. Kutokana na mazingira hayo ya matumizi mabaya ya fedha za serikali kwa safari za mara kwa mara za ndani na nje ya nchi, na malipo yanayofanyika kwa watumishi hewa katika orodha ya watumishi wa serikali nayo yalifanyiwa kazi. Kipindi cha uongozi wake yameibuka maneno ya misimu mbalimbali miongoni mwa maneno hayo ni ‘majipu’ ikimaanisha watu wasio

na sifa katika uongozi au watu wadanganyifu. Msimu huu unaelezea watu wanaoshindwa kutumia madaraka waliyopewa kwa vizuri hivyo huitwa jipu ikiwa na maana mtu huyo hafai katika uongozi. Mfano wa ujumbe ufuatao kupitia ukurasa wa mtandao wa instagram umeonyesha kabisa sababu mojawapo ambayo inasababisha maneno ya misimu kuibuka ni kutokana na matukio mbalimbali yanayoibuka katika jamii maneno yote ambayo yapo katika ujumbe huo yamebebwa na matukio tofauti yaliyoikumba jamii kwa nyakati tofauti kipindi cha mwaka 2017.




**Kielelezo 4.2: Misimu Iliyozungumzwa Zaidi 2017**

Chanzo: Ujumbe Instagramu, 2017

Kwa upande wa misimu inayotokana na mabadiliko ya kisiasa au zama tofauti za uongozi, hotuba ya kwanza ya Rais Magufuli bungeni ya Novemba 10, 2015 katika mikakati inayohusu utendaji wa kazi katika awamu yake, miongoni mwa maazimio ya mipango yake ni kutumbua jipu/majipu kwa watumishi watakaokwenda kinyume na maadili ya kazi, kama rushwa na ufisadi. Majadiliano yaliyofanyika kati ya mtafiti na watafitiwa pia yalihusu msimu wa ‘watumishi hewa’. Hivyo, watumishi hewa ni watumishi ambao mishahara yao inalipwa na halmashauri husika bila wao kuwepo kazini kwa utoro wa makusudi au kwa kuachishwa kazi, kufariki dunia au kufukuzwa kazi. Kuhusu suala hilo majadiliano hayo yaliweza kutoa mifano ya misimu ya watumishi hewa au wanafunzi hewa kulingana na muktadha. Hewa ni moja kati ya maneno ya misimu yaliyotumika kipindi cha sakata la wizi wa kutoa mikopo kutoka bodi ya mikopo kwa wanafunzi hewa yaani wanafunzi wasiokuwepo katika orodha ya wanafunzi kwenye vyuo vikuu. Pia kwa watumishi wa serikali waliokuwa wanalipwa fedha wakati hawapo kwenye orodha ya watumishi. Hivyo, tafsiri ya matokeo ya utafiti inaonesha kuwa maneno ya misimu hutokana na mabadiliko ya kihistoria katika nyakati tofauti kwenye jamii kama ilivyojitokeza katika kipindi cha utawala wa Raisi John Joseph Pombe Magufuli. Vilevile katika vipindi tofauti, nchi ya Tanzania iliingia katika mfumo wa vyama vingi ambapo inathibitika kuwa mfumo wa vyama vingi ni:

> “ni hali ya kuwa na chama zaidi ya kimoja, katika nchi moja. Na madhumuni ya kuwa na vyama vingi vya siasa ni kuleta ushindani wa kisiasa, ili kuleta maendeleo ya nchi. Hata hivyo upinzani wa kisiasa sio uadui bali ni kuongeza wigo wa demokrasia katika jamii husika.” (https//sw.m.wikipedia.org>wiki>orodhayaTanzaniana vyamavyasiasa)

Katika kipindi hicho yaliweza kuzuka maneno mengi ya misimu yaliyohusiana na matukio mbalimbali yaliyobainika. Maneno ya misimu yafuatayo yalijitokeza kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 4.5: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake Upande wa Kisiasa**

| Maneno ya Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| Ukawa | Kundi upande wa upinzani kati ya wanafunzi na wanafunzi |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Maneno ya misimu yaliyojitokeza katika kipindi hicho ni 'ukawa' likiwa na maana ya upinzani au wapinzani. Maana halisi ya neno ukawa ni kifupi cha Umoja wa katiba ya wananchi. Dhana iliyotokea wakati wa marekebisho ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2014, ambapo vyama vya upinzani waliunda umoja wao uliojulikana UKAWA. Watafitiwa walitumia neno la misimu 'ukawa' pale walipokuwa na upinzani kati ya wanafunzi wenyewe kwa wenyewe au katika mfumo husika. Hivyo, utafiti unathibitisha kuwa chanzo cha misimu kupitia majadiliano yaliyofanyika kuwa ni mabadiliko ya kisiasa nchini ambayo yamesababisha kuibuka kwa msimu wa ukawa miongoni mwa wanafunzi.

Aidha, chanzo cha misimu kulingana na majibu ya watafitiwa kupitia majadiliano imebainika pia kuwa mabadiliko ya kiutamaduni nayo yamechangia kuibuka kwa maneno ya misimu. Ikumbukwe kuwa utamaduni:

> "ni kama utaratibu wa jamii fulani, ambao wamekubali kuishi katika hali fulani ambayo huendana na mila na desturi za mahali husika. Kila jamii huwa na mila na desturi zao ambazo wamejiwekea".

(tanzanianculture2016.blogspot.comutamaduninininini,utamaduni wamtanzania)

Kila jamii katika taifa huwa na mila na desturi zao walizojiwekea ambazo huwatofautisha na jamii nyingine. Mfano, jamii ya watu wa kanda ya ziwa huwa na mila na desturi ambazo ni tofauti na watu wa ukanda wa pwani. Kanda ya ziwa ina makabila mengi, miongoni mwake ni wasukuma, Wajita, Wakerewe, Wanyambo na Wahaya. Makabila hayo humthamini sana mtoto wa kiume, hivyo wamejiwekea desturi zao kwa watoto wa kike au jinsia ya kike kusalimia wakiwa wamepiga magoti, au kitendo cha kumpa kitu mkubwa ni lazima jinsia ya kike ipige magoti. (Chanzo: Majadiliano ya wanafunzi 2017). Katika dhana ya utamaduni utafiti pia uliweza kubaini kuwa mwanaume ana jukumu kubwa katika familia. Sheria ya ndoa katika kifungu cha 9 cha sheria ya ndoa ya mwaka 1971, inadai kuwa mke au wake wana haki ya kutunzwa na mume wao kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama chakula, malazi, mavazi, matibabu nakadhalika. Mwanaume amepewa majukumu makubwa katika suala la kuangalia familia, hivyo anatakiwa afanye kazi ili kutimiza mahitaji ndani ya familia yake. katika vitabu vitakatifu, kama kitabu cha Mwanzo 2:15, neno la Mungu linasema Bwana Mungu akamtwaa mtu huyo, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. Dhana hii inatudhihirishia kuwa mwanaume ndiye mwenye majukumu makubwa katika kuhudumia familia tofauti na kipindi hiki cha karne ya ishirini na moja.

Kutokana na mabadiliko ya kiutamaduni siku hizi wanaume wanahudumiwa na wanawake, hii imejitokeza sana kwa wanaume wadogo kuhudumiwa na wanawake

watu wazima. Jambo hilo limeweza kuibua maneno ya misimu ambayo yanatumiwa sana kwenye mitandao ya kijamii kama jedwali lifuatalo linavyoonesha:

**Jedwali Na. 4.6: Orodha ya Maneno ya Misimu Upande wa Kiutamaduni**

| Maneno ya Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| Marioo | wanaume wanaolelewa na wanawake |
| Serengeti boys | vijana wadogo wa kiume wenye mahusiano ya kimapenzi na watu wazima |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Hivyo, kulingana na maneno ya misimu inadhihirisha kuwa mabadiliko ya kiutamaduni huibua maneno mapya yanayotumika katika jamii dhana ambayo inatumika sana katika mitandao ya kijamii. Kwa upande wa mabadiliko ya kiuchumi, ugumu wa maisha pia umekuwa ni chanzo cha kuibuka kwa maneno ya misimu katika jamii kama jedwali lifuatalo linavyofafanua:

**Jedwali Na. 4.7: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake Upande wa Kiuchumi**

| Maneno Ya Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| pambana na hali yako | Kuishi kulingana na ulichonacho/kipato chako halisi |
| vyuma vimekaza’ | Maisha kuwa magumu |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Maneno ya misimu hayo yameibuka kutokana na hali ngumu ya maisha iliyopo baada ya mianya yote ya fedha kuzuiliwa na serikali. Misimu hiyo inatuthibitishia kuwa kuna hali ngumu ya uchumi hivyo jamii ikubaliane na hali hiyo. Katika mabadiliko

ya kijamii watafitiwa wamebaini pia kuwa wasanii ambao ni sehemu ya wanajamii kupitia nyimbo zao wameweza kuibua misimu mbalimbali kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 4.8: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake Upande wa Kijamii**

| Maneno Ya Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| hana malinda' | Kuanza kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja, hususan kati ya mwanaume kwa mwanaume. |
| chura | Makalio makubwa (hii ni kwa wanawake wenye makalio makubwa) |
| Mrupo/dada poa | Mwanamke/msichana mwenye tabia ya umalaya |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Misimu hiyo inathibitisha kuwa wasanii ni chanzo cha kuibuka kwa misimu katika jamii. Mfano, Msimu wa hana malinda umejitokeza katika wimbo makalio wa Nay wa mitego kwenye wimbo wake wa Wapo na neno la misimu 'chura' ambalo limebeba dhana makalio makubwa na neno hilo la msimu lilianza baada ya msanii Snura Mushi kuimba wimbo wa chura kwenye miaka ya 2015/2016 Hata hivyo, maneno ya misimu mrupo au dada poa likiwa na maana ya mwanamke/msichana mwenye tabia ya umalaya. Dhana hii imeibuka kutokana na tabia ya wanawake au wasichana kuwa na tabia ya kufanya uasherati na kila mwanaume kwa nia ya kupata fedha. Watafitiwa waliibuka maneno ya misimu yaliyotokana na ujumbe tofauti tofauti za wasapu mfano hotuba ya Rais J.P. Magufuli mkoani Kagera watu waliweza kunukuu sehemu ya hotuba hiyo na kuirusha katika mitandao mbalimbali ya kijamii na iliwavutia kwasababu ndani yake kulikuwa na neno la msimu.

''ukiamua **kulibeba dude** …….. lazima watu wengine utawagusa''

(Chanzo: Mitandao ya kijamii 2017)

### 4.3 Matumizi ya Misimu Inayotumika Miongoni mwa Wanachuo

Nyangwine na Masebo (2002) wamebainisha matumizi ya misimu na kueleza kuwa ni kukuza lugha, kupamba lugha, kuibua hisia mbalimbali za wazungumzaji, hufurahisha, kuchekesha, hukosoa na kuiasa jamii. Misimu inayotumika mitandao ya kijamii inatokana hasa na masuala ya kimahusiano, masuala ya kisiasa na mambo mengine ya kiutamaduni. Massamba na wenzake (2009) wanaeleza kuwa watumiaji wa misimu huwa ni kikundi cha wazungumzaji wa lugha katika jamii ambao kimsingi huishi katika eneo moja. Kuzuka kwa misimu hutegemea mahitaji ya kikundi hicho kwa wakati huo mara mahitaji hayo yanapokwisha na misimu hutoweka. Hivyo, inadhihirisha kuwa kuna mahitaji makubwa sana ya misimu kutumika katika mawasiliano hususani katika mitandao ya kijamii. Misimu hiyo huwa na malengo tofauti kama vile kuficha/kufumba jambo, kukebehi nakadhalika. Misimu hutumika katika nyanja zote za maisha kama vile:

(i) kiuchumi mfano msimu kuchakachua, hapakazi tu, vyuma vimekaza

(ii) Kisiasa mfano kutumbua majipu, mwendokasi na ukawa

(iii) Kijamii mfano kiki, kuperuzi, mubashara, dada poa

Mtafiti aliwapa hojaji watafitiwa sitini kati ya watafitiwa themanini kutoka sampuli ya wanavyuo vitatu ili kuweza kupata taarifa sahihi ya maswali ya utafiti aliyoyaandaa. Maswali ya utafiti yaliyoandaliwa yalihusu kiasi cha utumizi wa maneno ya misimu ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Watafitiwa hamsini na saba kulingana na hojaji walizopewa waliweza kujibu swali hilo, tofauti na watafitiwa watatu waliobaki hawakuweza kujibu kabisa swali hili. Kielelezo kifuatacho kinaonesha majibu ya watafitiwa (waliojibu swali) kwa kuzingatia idadi na

asilimia katika swali linalohusu kiasi cha utumizi wa maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii. Majibu ya watafitiwa yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 4.9: Majibu ya Watafitiwa kwa Kuzingatia Idadi na Asilimia**

| **Idadi ya watafitiwa** | | **Majibu ya watafitiwa** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Wanaume | 05 | Kidogo | 05 | 8.3 |
| Wanawake | 05 | kidogo | 05 | 8.3 |
| Wanaume | 17 | Sana | 17 | 28.3 |
| Wanawake | 30 | Sana | 30 | 50 |
| Wanaume/ Wanawake | 03 | Hayatumiki kabisa | 03 | 05 |
| **Jumla** | **60** | | **60** | **100** |

Chanzo: Utafiti. 2017

Kutokana na majadiliano na hojaji zilizotolewa kwa watafitiwa, majibu ya watafitiwa kuhusiana na matumizi ya misimu inavyotumika katika mitandao ya kijamii imebainika kuwa rika ambalo lina matumizi makubwa ya misimu ni kundi lenye umri kuanzia miaka 18- 45. Jibu hilo limetokana na dodoso ambalo mtafiti amelitumia kutokana na swali lililouliza kwa watafitiwa kuwa ni rika gani hupendelea kutumia misimu. Utafiti uliweza kubaini hivyo kwa kuwa ndilo kundi lenye watumiaji wakubwa wa mitandao ya kijamii kulingana na mazingira yao ya vyuoni.

Matumizi hayo yametokea ili kuweza kuficha jamii nyingine tofauti na vyuoni wasiweze kuelewa jambo linaloongelewa, na pia huleta mvuto katika mawasiliano yao kwa njia ya mitandao ya kijamii. Ikumbukwe kuwa vijana au kundi la umri kati ya

miaka hiyo ambao ni wanavyuo ndio watumiaji wakubwa wa misimu kulingana na muktadha husika. Hivyo, sababu za kimazingira kama vile kijiweni ambapo kumeweza kuibua maneno kama sepa, mshikaji, demu, mzuka nakadhalika ambazo ni sababu kuntu zilizochangia kundi hili kuwa watumiaji wakubwa wa mitandao ya kijamii.

Kwa kiasi kikubwa cha wanavyuo hupenda kukaa vijiweni kwa kuwa ni kundi rika moja na kuibua maneno ya misimu ambayo huyatumia kulingana na mazingira yao. Mfano wa misimu iliyoibuliwa kutokana na kundi hili la vijana wakiwa pamoja ni kama vile 'mtu wangu','mchepuko','mshikaji','kimenuka','sepa' nakadhalika. Hata hivyo, watafitiwa walieleza kuwa:

> "Matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii ni ya kiasi kikubwa kwa kuwa watumiaji wengi hujikuta/hupendelea kutumia maneno yasiyo rasmi katika mitandao hiyo"
>
> (Chanzo: Majadiliano ya wakufunzi 2017)

Matumizi ya maneno ya misimu yamekuwa kwa kiasi kikubwa kutokana na aina za misimu inayotumiwa. Mfano kuna misimu inayotumiwa na sehemu kubwa ya jamii kutokana na tukio ama wakati, wengine hutumia kutokana na ukaribu mathalani ndugu, marafiki wafanyakazi kwa pamoja mfano grupu za 'whatsaap', uso wa kitabu. Kuna aina nyingi za misimu inayotumiwa na watu wengi katika jamii ambayo imetokana na mabadiliko ya kihistoria katika jamii. Mfano, nchi ya Tanzania kuna maneno mengi ya misimu yaliyoibuka kulingana na matukio mbalimbali yaliyotokea katika jamii kama jedwali lifuatalo linavyofafanua:

**Jedwali Na. 4.10: Orodha ya Maneno ya Misimu Kulingana na Matukio Tofauti**

| Maneno ya Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| Makinikia | Mchanganyiko wa vitu fulani |
| Bashite | Mtu aliyepata daraja sifuri |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Msimu wa neno makinikia unatumika sana katika jamii kuonesha mchanganyiko wa vitu fulani. Msimu huu umejitokeza mara baada ya sakata la kukamatwa kwa makontena eneo la bandarini yakiwa na mchanga wenye madini tofauti, ambapo miongoni mwa madini hayo ni dhahabu, copper, silver, sulphur, chuma nakadhalika. Mchanga huo baada ya uchunguzi ulionekana una madini tofauti na ulikuwa uko tayari kupelekwa nchi za nje. Hivyo kwenye mitandao ya kijamii kumekuwa na matumizi makubwa ya neno ‘makinikia’. Vilevile, chakula kinachoitwa pilau (BAKITA 2017:886) anaeleza kuwa pilau ni chakula ambacho hupikwa kwa kuchanganya mchele na viungo kama binzali nyembamba, mdalasini, iliki, pilipili manga na nyama au samaki. Kutokana na dhana hiyo neno pilau limepewa jina la makinikia kwa kuwa chakula hicho kina mchanganyiko wa mchele, nyama na viungo mbalimbali.

Hivyo basi misimu hutumika sana katika mitandao ya kijamii kulingana na hizo aina tatu za misimu ambapo kuna misimu ya kipekee hii inatumika na kikundi fulani cha watu, misimu zagao hii ipo katika eneo kubwa mathalani nchi nzima mfano wa misimu zagao vyuma vimekaza, mchepuko, sepa kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Aina hii ya misimu inatumika popote pale nchini Tanzania watumiaji wa mitandao ya kijamii wakikutana na misimu hii huelewa dhana inayokusudiwa. Mwisho ni misimu

tarafa ambayo inatumika katika eneo dogo kama vile ‘mbwari’ ni neno la misimu linalotumika katika tarafa mojawapo mkoani Morogoro hususani kata ya Mlali wilayani Mvomero wakati wazee au vijana wawapo kwenye vilabu vya kunywa pombe. Neno ‘mbwari’ likiwa na maana ya pombe ya kienyeji inayonywewa katika eneo hilo. Neno lingine ni ‘makontena’ likiwa linatumiwa zaidi kwenye taasisi za elimu hasa vyuo likimaanisha kuwa kuna awamu nyingine ya wanafunzi wanaokuja kwa ajili ya kuanza mafunzo katika vyuo hivyo.

**Tafsiri ya Matokeo**

Mtafiti katika kupitia maswali ya dodoso ameweza kubaini kuwa maneno ya misimu yanatumika sana katika mitandao ya kijamii. Kutokana na swali linalohusu kwanini misimu inatumika sana? Swali ambalo limejibiwa kwa asilimia 90 na watafitiwa na majibu yao yalibaini kuwa misimu hurahisisha mawasiliano miongoni mwa makundi rika yanayotumia mitandao ya kijamii, misimu husaidia kuficha siri kwa jambo linaloongelewa. Mfano wa neno la msimu ‘amsha dude,’ ‘toa malinda’, maneno haya yanapotumiwa watumiaji huwa na lengo la kuficha uhalisia wa jambo kwa kupunguza ukali wa maneno. Utafiti bado uliendelea kubaini kuwa wanaaongoza katika matumizi ya mitandao ya kijamii ni vijana hasa wenye umri wa miaka 12-35 na 35- 45. Makundi hayo huongoza kwa kuwa kwao huona rahisi kutumia misimu katika kurahisisha mawasiliano miongoni mwao, kasumba, kutaka usasa, usiri wa jambo lizungumzwalo na kuficha siri hizi ni sababu zilizobainishwa na watafitiwa ambazo zinasababisha rika nililoainisha hapo juu kutumia zaidi maneno ya misimu na wakati mwingine huhitaji kundi dogo kuweza kuelewa maana ya hiyo misimu jinsi iliyotumika.

Kwa kupitia majibu ya watafitiwa, mtafiti amebaini aina zote za misimu hutumika katika mitandao ya kijamii na huanza katika eneo dogo na baadae huweza kuongeza mawanda ya kimatumizi na hiyo imejidhihirisha katika orodha hakiki ambayo mtafiti aliwapa watafitiwa. Matokeo yanaonesha kuwa jumla ya orodha hakiki 40 zilijazwa na watafitiwa tofauti kutoka vyuo vitatu na miongoni mwa hayo maneno na matumizi yake yaliandikwa sawa kutoka kwa watafitiwa. Pia, imebainika kuwa kulikuwa na maana zinazofanana pamoja na matumizi yake, dhana zilizoweza pia kubainishwa na Nyangwine na Masebo (walikwishatajwa).

**Jedwali Na. 4.11: Orodha ya Maneno Yaliyoandikwa na Idadi Kubwa ya Watafitiwa**

| Misimu | Matumizi |
|---|---|
| Matumishi hewa | Hutumika kuashiria watumishi wasio halisi |
| Kutumbua majipu | Kutoa uozo ua uharibifu katika taasisi au mashirika ya umma |
| Hapa kazi tu | Huashiria ufanyaji kazi kwa bidii |
| Amsha dude | Kuibua jambo |
| Pambana na hali yako | Kabiliana na changamoto kutokana na mahitaji yako |
| Mubashara | Matangazo ya moja kwa moja |
| Kukwea pipa | Panda ndege |
| Sakata | Jambo lisilo la kawaida |
| Bifu | Uhasama |

Chanzo: Kutoka Uwandani, 2017

Kutokana na kielelezo hapo juu utafiti umebaini baadhi ya maneno yanayotumiwa sana katika mitandao ya kijamii katia kipindi cha hivi karibuni na watafitiwa. Hata

hivyo, utafiti umeendelea kubaini kuwa watumiaji wa mitandao ya kijamii wanayatumia kwa kiasi kikubwa zaidi ya asilimia 85. Miongoni mwa watumiaji wa mitandao ya kijamii, misimu imekuwa ni kama maneno maalumu ya kuwasaidia kuwasiliana kwani kwa kurejea aina za misimu wanaweza kuwasiliana kwa kuchagua hadhira ya kuwasiliana nayo kwa wakati husika Mfano maneno ya misimu'amsha dude' kupitia istagramu kuna ujumbe usemao:

> "Msanii Roma Mkatoliki kuamsha dude tena".
>
> (Chanzo: Ujumbe wa instagramu 12:50 10/10/2017)

Kutokana na ujumbe huo sio wasomaji au watumiaji wa ukurasa ule wa istagramu wataelewa dhana au ujumbe uliokusudiwa kwenye hiyo sentensi, bali wachache ndio watakaoelewa maana hiyo kuwa Roma Mkatoliki anaweza kuibua jambo jingine jipya ambalo litamfanya watu wafuatilie. Utafiti uliweza kubaini pia mfano wa ujumbe mwingine kutoka mitandao ya kijamii kwa upande wa wasapu nao ulisema:

> "Unavyonitongoza hivyo una mashine lakini?
>
> Sio unanipotezea muda afu una kibamia."
>
> (Chanzo: Ujumbe wa wasapu 12:37, 6/11/2017)

Maana ya ujumbe huo utapokewa sana na wachache sana kundi la vijana na kushindwa kueleweka kwa wengine. Ujumbe huo ulikuwa unamaanisha kuwa aliyetuma ujumbe huwa ni wa jinsia ya kike, na anamuasa anayemfuatilia kuwa je ataweza kazi katika tendo la ndoa, na isije kuwa ana uume mdogo (kibamia) atampotezea muda.

Katika kuangalia matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii, mtafiti ili aweze kupata data sahihi aliweza kuwapa watafitiwa dodoso sitini (80). Hata hivyo, kati ya dodoso hizo zilizojazwa na kurejeshwa ni sabini na tano (75) na dodoso tano hazikuweza kurejeshwa na orodha hakiki ya maneno ya misimu na matumizi ya hayo maneno katika mitandao ya kijamii ziliweza kujazwa na sampuli yote ya wanachuo lakini maneno hayo mengi yalionekana kujirudia kutokana na kufanana kama inavyoonekana kwenye kiambatisho Na. 02. Lengo la mtafiti ni kuweza kufahamu maneno ambayo watafitiwa wanayatumia sana katika mitandao ya kijamii na maana zake. Utafiti ulichambua maneno hayo na kupata takribani maneno 250 ambayo yamejitokeza sana kwenye orodha hiyo. Uchambuzi huo unadhihirisha kuwa matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii ni wa kiasi kikubwa kwa asilimia zaidi ya 85 ukilinganisha na maneno mengine.

Aidha, matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii inatumika kwa kiasi kikubwa na hii imechangiwa pia na sera mpya iliyoandaliwa na TCRA inayodhibiti matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii ikiwepo katazo la lugha ya matusi kupitia mitandao ya kijamii. Hivyo, watafitiwa wakabaini kuwa watumiaji wakaona waje na mbadala wa kutumia maneno ya misimu ili kupunguza ukali wa maneno na pia kutoa na kueleza hisia zao katika mitandao. Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya maneno ya misimu.

**Jedwali Na. 4.12: Orodha ya Maneno ya Misimu Miongoni mwa Wanachuo**

| Maneno ya Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| Hawana malinda | Wanaume wanaojihusisha na maapenzi kinyume cha maumbile |
| Wanatoa tigo | Wanawake wanaojihusisha na mapenzi kinyume cha maumbile |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Misimu hiyo imefanya kazi ya kuficha ukali wa maneno badala ya kuongea maneno halisi yametumika maneno ambayo ni vigumu jamii isiyo karibu na jamii ya wanavyuo hao kuelewa. Mfano pale wanapotaka kuzungumzia wanaume wanaojihusisha na mapenzi kinyume na maumbile wakiwaita majina **“hawana malinda”** au wanawake ambao wanajihusisha na hiyo tabia ya kufanya mapenzi, wao huitwa **“wanatoa tigo”.** Kulingana na maneno mbalimbali ya misimu inavyotumika katika mitandao ya kijamii na maana zake, inatutanabaisha kuwa misimu imetumika kupunguza ukali wa hayo maneno. Kupitia utafiti huu majibu ya watafitiwa yaliweza kubainisha matumizi ya misimu kama vile:

> “Misimu inatumika kukuza lugha kwa kuwa baadhi ya misimu ilikuwepo zamani na iliweza kutumika na baadae ikatumika kama msamiati wa lugha ya Kiswahili mfano neno shangingi. ”
> (Chanzo: hojaji ya wanachuo 2017)

Katika utafiti huu, Kupitia majibu ya dodoso misimu pia imethibitika kuwa misimu hutumika kuweka usiri wa jambo linalozungumziwa kwenye mitandao ya kijamii kama jedwali lifuatalo linavyofafanua:

**Jedwali Na. 4. 13: Orodha ya Maneno ya Misimu katika Kuficha Siri wa Jambo**

| MANENO YA MISIMU | MAANA ZAKE |
|---|---|
| kimenuka | Mambo yameharibika au kufichuka |
| kutoa malinda | Mapenzi ya jinsia moja |
| Mkulu/daddy | Kiongozi mkubwa wa nchi |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Maneno ya misimu hapo juu inaonesha kuwa misimu inatumika kuficha siri mfano ‘kimenuka’ ikiwa na maana ya mambo yameharibika iwapo kulikuwa na jambo lililofichika sasa limefichuka, ‘kutoa malinda’ ikiwa na maana ya mapenzi ya jinsia moja. Vilevile, iwapo anazungumziwa kiongozi mkubwa wa nchi wazungumzaji hawamtaji moja kwa moja bali wanaita ‘mkulu’, ‘Daddy’ nakadhalika. Aidha, misimu hii ukiitumia watumiaji huweza kuficha siri au kuweka sitara kwa hayo maneno maana ukiyatumia waziwazi huwa yanakuwa na ukali na si sahihi kuyasema wazi mbele za watu.

Kupitia majibu ya watafitiwa misimu pia hutumika “kupamba lugha” kwa watumiaji wa mitandao ya kijamii hutumia misimu kuweza kuipamba lugha na kufanya ujumbe na mada zinazochangiwa kupitia mitandao ya kijamii zinavutia kwa kuchopeka hayo maneno. Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya misimu kuonesha kuwa ina kazi ya kupamba lugha.

**Jedwali Na. 4.14: Orodha ya Maneno ya Misimu katika Kupamba Lugha**

| **Maneno Ya Misimu** | **Maana Zake** |
|---|---|
| Pambana na hali yako | Vumilia na kupambana ili ufanikiwe |
| Amsha dude | Amua kusema baada ya maudhi ya muda mrefu |
| Jaza ujazwe | Tumia fedha kidogo, uwekewe nyingi zaidi |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa, 2017

Maneno ya misimu hiyo inaonesha kuwa inavutia au kufurahisha kulingana yanvyotumika kwa kuzingatia muktadha husika. Mfano wa hiyo misimu ‘pambana na hali yako’ ikiwa na maana kuwa haijalishi uko katika kipindi kigumu cha fedha au

mambo mengine, huna budi kuvumilia na upambane ili uweze kufanikiwa. Msimu huu umekuwa ukitumika sana na vijana kulingana na kuwa na hali ngumu ya fedha iliyosababishwa na kukosa mikopo ya bodi ya mikopo. Msimu 'amsha dude' ikiwa na maana kuwa kama mtu aliamua kukaa kimya wakati anachokozwa, mwishowe anaamua kusema baada ya maudhi ya muda mrefu. Vilevile, msimu 'jaza ujazwe' ukiwa na maana weka fedha kidogo ili uwekewe nyingi zaidi au ukiweka akiba fedha ndio utapata zaidi. Msimu mwigine ni makinikia ukiwa na maana ya kuwa na mchanganyiko wa vitu vingi kwa wakati mmoja/ kwa mara moja. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa ujumbe unaoandikwa kwenye mitandao ya kijamii hutumia sana maneno ya misimu ambayo huvutia na hufurahisha watumiaji.

## 4.4 Changamoto za Kutumia Misimu katika Mitandao ya Kijamii Miongoni mwa Wazungumzaji

Kulingana na majibu ya watafitiwa kupitia hojaji na maswali ya majadiliano utafiti umeweza kubainisha changamoto zinazowakabili wazungumzaji katika matumizi ya maneno ya misimu kwenye mitandao ya kijamii. Watafitiwa waliweza kupewa hojaji ambazo zimemsaidia mtafiti kupata data sahihi kulingana na utafiti wake.

Hojaji alizozigawa mtafiti zilikuwa jumla ya hojaji mia moja na ishirini (80) Kati ya hojaji hizo, hojaji sabini na tano (75) zilikuwa na majibu kutoka kwa watafitiwa wanachuo wa sampuli ya Chuo A, sampuli ya Chuo B na sampuli ya Chuo C. Pamoja na hayo, kulikuwa na majibu kutoka sampuli ya chuo C ambayo yaliwajumuisha wakufunzi 07. Kutokana na hojaji hizo kupitia sampuli tatu, kati ya hojaji hizo 60 ndizo zilirudi na ilijumuisha hojaji moja kutoka sampuli ya Chuo C ambayo haikujazwa chochote.

Kielelezo kifuatacho kinaonesha idadi ya hojaji zilizojazwa na zilijibu swali Na. 13 kama inavyoonekana kwenye kiambatisho Na 01 ambayo maswali haya yalikuwa yanajibu changamoto za kutumia misimu katika mitandao ya kijamii.

**Jedwali Na. 4.15: Idadi ya Hojaji Zilizojazwa**

| Kundi lengwa | Sampuli chuo A | Sampuli chuo B | Sampuli chuo C | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| wanachuo | 25 | 25 | 25 | 75 |
| wakufunzi | | 06 | 10 | 16 |
| **Jumla** | **25** | **31** | **35** | **95** |

Chanzo: Kutoka Uwandani, 2017

**Tafsiri ya Matokeo**

Kutokana na majibu ya watafitiwa kupitia hojaji watafitiwa kwa kiasi cha asilimia zaidi ya themanini (90 ) walikubali kuwa kuna changamoto za kutumia maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii. Utafiti uliweka majibu hayo kwa kufuata hatua mbili ambapo katika hatua ya kwanza uliangalia majibu ya watafiti na changamoto zake kwa kuzingatia sampuli ya chuo A, chuo B na chuo C.

**Hatua ya kwanza**

Majibu ya sampuli kutoka Chuo A yaliweza kubainisha changamoto za kutumia misimu katika mitandao ya kijamii kama ifuatavyo:

(i) Misimu inapotosha mawasiliano

(ii) Inasababisha ujumbe kutofika kwa walengwa iwapo hawajui maana ya misimu husika.

(iii) Inaleta lugha ya matusi

(iv) Inaharibu matumizi ya lugha

Hizi ni baadhi ya changamoto ziliozobainishwa na watafitiwa wengi kutoka sampuli ya Chuo A. Sampuli ya Chuo B changamoto zilizobainishwa na watafitiwa ni:

(i) Kushindwa kupata ujumbe

(ii) Kutokueleweka kwa maana za misimu.

(iii) Maneno ya misimu hudumu kwa muda mfupi.

(iv) Hupelekea ugomvi au kutokuelewana miongoni mwa watu.

Kutoka sampuli ya Chuo C, majibu ya watafitiwa kuhusiana na changamoto waliyoibainisha ni:

(i) Kutokueleweka kwa maana iliyokusudiwa katika misimu husika.

(ii) Kutokuelewa dhana iliyozungumzwa.

(iii) Kubadilikabadilika kwa misimu. Dhana hii inawafanya watafitiwa kushindwa kuitumia misimu kwa kuwa husababisha ujumbe kubadilika. Mfano wa neno la misimu shangingi neno hili limetokana na maana yake halisi ikimaainisha aina ya gari la kifahari. Aidha, neno hili likaongezewa matumizi na linatumika kwa kuwaita wanawake wenye tabia ya kuwa na wanaume wengi na wanaopenda pesa kuwa ni mashangingi.

**Changamoto za Matumizi ya misimu katika Mitandao ya Kijamii**

Hata hivyo, utafiti uliweza kubaini changamoto za kutumia mitandao ya kijamii kutokana na mahojiano aliyoyafanya mtafiti na watafitiwa ambao ni wakufunzi na wahadhiri kutoka sampuli ya vyuo vitatu. Kwa jumla, misimu ilionekana ina changamoto zifuatazo ambazo zilihusu mambo yafuatayo:

(i) Misimu ina chumvi nyingi hivyo huweza kusababisha ujumbe kutokueleweka

(ii) Hufanya majungu

(iii) Hukwaza mawasiliano

(iv) Hufanya lugha kudumaa

(v) Hupunguza hadhira katika mitandao, hutengua mawasiliano, maneno yasiyoaminika katika jamii.

Kutokana na utafiti huu imebainika wazi kuwa hizo ndizo changamoto walizozibainisha watafitiwa kupitia hojaji na majadiliano kupitia sampuli ya vyuo vitatu Morogoro.

**Hatua ya pili**

Utafiti pia, ulibainisha hatua ya pili ambayo ni kuorodhesha maneno ya misimu yanayotumika katika mitandao ya kijamii pamoja na maana zake. Hata hivyo, kulingana na watafitiwa waliwea kupakua ujumbe wa 'whatsaap' ufuatao pamoja na maana yake kulingana na muktadha:




**Kielelezo 4.3: Dhana ya Msimu Mchepuko**

Chanzo: Ujumbe Whatsaap, 2017

Kutokana na majibu ya watafitiwa, utafiti uliweza kubaini maana tofauti kulingana na muktadha husika. Ufafanuzi wa maana ya Ujumbe wa 'whatsaap' kutoka sampuli ya vyuo vitatu uliweza kubaini maana ya ujumbe huo kwa maana na mitazamo tofauti. Fasili za ujumbe huo zilitofautiana kimitazamo kama ifuatavyo:

**Fasili ya Chuo A**

Sampuli hii ilifasili kuwa katika nchi ya Tanzania iwapo mtu akiingiza mali ya magendo au vitu vingine kinyume cha sheria hata iwe usiku taarifa zitawafikia watu. Lakini, iwapo mtu akija kuiba mali hata iwe mchana watu wataendelea na shughuli zao kana kwamba hawakuona mali ikiibiwa.

**Fasili ya Chuo B na C**

Ujumbe huu pia unaweza kufasiliwa tofauti kulingana na muktadha wa kijamii. Katika muktadha huo ulifasiliwa kuwa watu huwa makini kuangalia kama mwanaume anatembea na mwanamke ambaye siye mke wake (mchepuko) tendo hilo laweza kutokea wakati wa mchana au usiku lakini watu hao lazima watajua tu. Kwa upande mwingine, mwizi au kibaka anapoingia ndani ya nyumba ya mtu na kutaka kuiba wakati wa mchana hakuna mtu atakayejua kwa kuwa kila mtu ana shughuli zake. Kutokana na ujumbe huo inabainisha kuwa kuna changamoto kubwa katika kuelewa dhana ya misimu kutokana na utafiti huu, kwani kila mtu huja na fasili zake kufuatana na muktadha husika. Mfano mwingine kupitia ujumbe wa instagram Millardayo unasema kuwa:

> 'bora maumivu ya kuachwa na mademu watatu kuliko
> maumivu ya kukuta missed Call 3 za tatu mzuka'
> (kutoka millardayo hayo 17/11/2017)

Ujumbe huu unaweza kufasiliwa katika mitazamo tofauti kulingana na muktadha. Utafiti pia, ulibaini kuwa misimu huwa inaathiri jamii kwa kuwa inakuwa na matusi mfano neno ‘toa malinda’ na nipe tigo kama ilivyokwisha elezwa katika kipengele cha 4.2. Maneno hayo maana zake sio nzuri iwapo mtu atataka kujua zaidi maana hiyo, huwa inaathiri watu. Vilevile utafiti ulibaini kuwa kuna baadhi ya misimu haieleweki kabisa kwa watumiaji, mfano wa misimu ifuatayo ambayo inatumika sana kwenye mitandao ya kijamii katika kipindi hiki kama jedwali linavyofafanua:

**Jedwali Na. 4.16: Orodha ya Maneno ya Misimu na Maana Zake**

| Maana Za Misimu | Maana Zake |
|---|---|
| Vyuma vimekaza | Hali ngumu ya kifedha |
| Jamaa mawe anayo | Jamaa ana fedha nyingi |

Chanzo: Majibu ya Watafitiwa 2017

Kutokana na jedwali hilo inathibitisha kuwa mifano hiyo ya misimu imekuwa ikitumiwa sana na watu katika mitandao ya kijamii. Mfano kama jedwali linavyofafanua kuwa ‘vyuma vimekaza’ msimu huu unatumika sana kipindi hiki cha awamu ya tano ya uongozi wa Rais John Joseph Pombe Magufuli kuwa fedha iliyokuwa inapatikana kwa njia zisizo halali sasa upatikanaji wake umekuwa mgumu kwani mianya iliyotumika kupata hizo fedha imedhibitiwa (imezibwa).

Hivyo, fedha imekuwa ngumu kupatikana na hali ya maisha imekuwa ngumu. Maneno ya misimu ‘jamaa mawe anayo’ ikiwa na maana jamaa ana fedha nyingi, neno mawe limesimama badala ya fedha ni misimu inayotumika sana katika jamii. Kutokana na utafiti uliofanyika imebainika kuwa lengo kubwa katika majadiliano hayo na mifano iliyotolewa kutoka jumbe mbalimbali za ‘whatsaap’ ni kubaini namna maneno hayo yanavyotumika na maana zake.

**Changamoto za Matumizi ya Misimu**

Majibu ya watafitiwa kuhusu changamoto za kutumia misimu kutoka katika maswali ya dodoso ambayo mtafiti aliwapata watafitiwa waliweza kubainisha changamoto zifuatazo:

(i) Misimu ina chumvi nyingi kupitia majibu yao katika dodoso na majadiliano waliweza kueleza ni kwa namna gani misimu ina chumvi nyingi mfano maneno ya misimu kama‘ ana mawe’ likiwa na maana ana pesa nyingi ‘mubasharaha’ likiwa linatumika kuwekea mkazo wa jambo au habari kupitia matangazo ya moja kwa moja.

(ii) Inaua lugha watafitiwa pia waliweza kueleza misimu inaua lugha kupitia majibu ya watafitiwa maneno mengine ya misimu yanatumika katika jamii yakiwa na maana nyingine ila yanageuzwa matumizi na maana pia mfano ‘mpe tigo’ ‘ toa malinda’.

(iii) Inasababisha mawasiliano kutofika kwa ufanisi kwa wahusika.

Kupitia majibu ya watafitiwa wakati wa majadiliano, wameona misimu inaweza kusababisha mawasiliano kutofika kwa usahihi au ufanisi mfano watumiaji wa mitandao ya kijamii kutumia maneno kama ‘mukulu’ likiwa na maana Rais wa Nchi sio rahisi dhana hii kueleweka katika ujumbe kupitia watu wote watakaosoma. Mfano wa ujumbe wa whatsaap:

> ‘jana nilimdanganya mke wangu nasafiri naenda Mbeya kumbe nipo tu kwa mchepuko kwa bahati mbaya leo mchana ile napanda daladala tegeta nikapishana nae mlangoni unajua niliiishiwa nguvu nikajikuta tu namuuliza mke wangu umenifuata mpaka Uyole’.

Huu ni ujumbe ambao watafitiwa waliunukuu katika majadiliano kupitia mtandao wa wasapu, ujumbe huu unaweza usieleweke kwa urahisi kwa watu wote watakaousoma kutokana tu na matumizi ya neno mchepuko wakati msimu huo una maana ya mwanamke asiye mke wake bali ni hawara.

Chanzo: Majibu ya watafitiwa kupitia majadiliano 2017)

(i) Huweza kusababisha migogoro iwapo mtu kapokea ujumbe kwenye mtandao na akashindwa kuuelewa hivyo akahisi ametusiwa au kudhihakiwa mfano 'amsha dude' 'demu'.

(ii) Hupotosha maana halisi ya ujumbe.

(iii) Wajifunzaji wageni kushindwa kujifunza lugha kwa ufasaha kutokana na majibu ya watafitiwa kuhusiana na changamoto walibainisha changamoto hiyo kwani iwapo watumiaji wengi wa mitandao ya kijamii wakitumia lugha yenye maneno mengi ya misimu ni vigumu wageni au wajifunzaji wapya wa lugha wanaotumia zaidi mitandao ya kijamii kama njia mojawapo ya kurahisisha mawasiliano yao wakaelewa na wakaweza kujifunza kikamilifu

Chanzo cha utafiti kupitia majadiliano 2017)

(iv) Maneno ya misimu huweza kuwaathiri watumiaji kwa kufikisha ujumbe usio rasmi au ujumbe kumfikia mtu asiye rasmi mfano wa misimu amsha dude, kula mzigo Kushindwa kupata maana halisi ya misimu inayotumika mfano Serengeti boys, marioo 'Baadhi ya maneno huleta ukakasi katika matumizi na kwa wasikilizaji mathalani jazwa ujazwe neno hili la msimu hutumiwa na rika la vijana likitafsiriwa kwa namna tofauti kwani wengi huusisha na masuala ya mahusiano ya kimapenzi'. (Chanzo majibu ya dodoso 2017).

(v) Lugha kuonekana kama ya kihuni hii ni mojawapo ya changamoto wanayokumbana nayo watumiaji wa mitandao ya kijamii kutokana na kutumia maneno ya misimu watafitiwa walibainisha maneno kama ‘sepa’ ‘dingi’‘ demu’ ‘kicheche’ haya ni baadhi ya misimu inayofanya lugha kuonekana kama ya kihuni na kuishusha hadhi yake.

(vi) Misimu husababisha watu kushindwa kuelewana kutokana na hayo matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii mfano ‘jazwa ujazwe’ dhana ya msimu huu inaweza kutafsiriwa tofauti kulingana na muktadha wa watumiaji katika mawasiliano na unaweza kusababisha watumiaji kutoelewa dhana au kuitumia tofauti.

(vii) Misimu pia huaribu matumizi ya lugha watafitiwa waliona hii ni mojawapo ya changamoto ya kutumia maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii ambayo husababisha kuharibu matumizi ya lugha. Mfano maneno kama ‘toa malinda’ ‘nipe tigo’ maneno haya yana maana halisi katika lugha lakini watumiaji huyatumia tofauti na kubadili kabisa dhana iliyokusudiwa yanatumika kumaanisha mahusiano ambayo ni tofauti na kawaida. Hivyo matokeo yake maneno haya pia husababisha utata.

**Tafsiri ya Matokeo Kuhusiana na Changamoto za Kutumia Maneno ya Misimu**

Kupitia majibu ya dodoso na majadiliano kupitia swali lililouliza kuhusu changamoto wanazokutana nazo watumiaji wa mitandao ya kijamii wanapokuwa wanafanya mawasiliano. Katika kujibu swali hili, pamoja na kuwa mtafiti ni naye aliweza kusoma baadhi ya ujumbe kupitia mitandao ya kijamii ameweza kubaini watumiaji wa mitandao ya kijamii wanakumbana na changamoto kadhaa kwa kutumika kwa misimu katika mitandao ya kijamii ikiwa ni pamoja na:

(i) Kukwamisha mawasiliano baina ya upande mmoja na mwingine kutokana na matumizi ya lugha ya mafumbo kama mukulu, bashite, vilaza, wahenga nakadhalika ambayo haieleweki miongoni mwa watumiaji wa mitandao hiyo ya kijamii.

(ii) Kuwa na ukakasi katika lugha. Mfano vyuma vimekaza, majipu, hewa inaweka ukakasi katika lugha kwa sababu maneno hayo ya misimu kuwa na maana tofauti na ile inayotumika kila siku.

(iii) Kuweza kusababisha ugomvi baina ya jamii kwa sababu baadhi ya misimu hiyo hudharirisha au kutumia lugha ya matusi mfano demu, kicheche, boya, jaza ujazwe, toa tigo, ana mawe.

(iv) Husababisha kutokuwa na uelewa mzuri wa ujumbe unaotumwa kupitia mitandao ya kijamii au kila mmoja kuwa na tafsiri yake mfano neno la msimu‘ ubuyu’ likiwa na maana ya umbea lakini tayari neno hili lina maana yake halisi kuwa ni chakula kinachoweza kuliwa chenye vitamini. Watumiaji ambao watakumbana na neno hili kupitia mitandao ya kijamii wanaweza kushindwa kupata ujumbe au tafsiri mahususi. Maneno ya misimu yakitumika katika mitandao ya kijamii baadhi ya watumiaji wa mitandao hiyo hushindwa kutafsiri vema ujumbe uliomo na matokeo yake huweza kupuuza ujumbe husika.

(v) Watumiaji kuchukizana na kuingia hatiani kutokana na makosa ya kimtandao kwa kuonekana wakitumia lugha ya matusi au kihuni. Mfano wa maneno kama demu, mshikaji, buzi, maneno haya yanapotamkwa tu huwa na ukakasi hivyo kupelekea kuibua hisia tofauti miongoni mwa watumiaji wa mtandao wowote wa kijamii.

### 4.5 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kuchambua data zilizokusanywa juu ya "kuchanganua chimbuko na matumizi ya Misimu katika mitandao ya kijamii pamoja na changamoto zake kwa wazungumzaji wa lugha ya kiswahili". Data zote zilizokusanywa kwa njia ya hojaji, mahojiano, uchunguzi na usaili zimewasilishwa. Utafiti ulibaini kuwa misimu itumikayo katika jamii hutokea kutokana na mabadiliko ya kihistoria au tukio linalojitokeza katika jamii. Tukio hilo huibua maneno ambayo huibuka na kuwa misimu. Hata hivyo, misimu itumikayo katika mitandao ya kijamii huweza kuleta kutoelewana baina ya makundi ndani ya jamii, mtu na mtu au kati ya jamii moja na nyingine. Hata hivyo, kutokana na data zilizokusanywa inaonesha kuwa misimu hutokea kulingana na mabadiliko ya kihistoria, au tukio linalojitokeza katika jamii. Sura inayofuata itaeleza kuhusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imejumuisha mada kwa upekee kwa kuonyesha matokeo na kuonyesha hitimisho ambalo limechorwa kutoka kwenye matokeo na kutoa mapendekezo kwa ajili ya tafiti zijazo elimu zaidi.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Mada ya Utafiti

Mada iliyotafitiwa ya kuchunguza chimbuko, matumizi ya maneno ya misimu na changamoto zake katika mitandao ya kijamii miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umefanyika katika wilaya mbili zinazopatikana katika mkoa wa Morogoro ambazo ni Morogoro mjini na Mvomero kwa kuhusisha vyuo vitatu Chuo kikuu Cha Kiislamu Morogoro, Chuo cha Ualimu Morogoro, Chuo Cha Ualimu Muhonda mtafiti aliamua kujikita kukusanya data katika vyuo hivi ni kwa sababu vimemsaidia sana mtafiti kupata taarifa alizozikusudia.

## 5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

### 5.3.1 Lengo la Kwanza la Utafiti

Lengo la kwanza la utafiti ni kubainisha chimbuko la kutumia misimu ambalo ni misimu huzuka kama utani na hutokana na matukio, wakati na mabadiliko yanayojitokeza mara kwa mfano mabadiliko ya kisiasa haya ni mabadiliko yanayotokana na vipindi vya utawala kama vile miaka ya 1985 hadi 1995 maneno ya misimu kama ruksa, miaka ya 1995-2005 maneno kama ngangari, ngunguri kipindi cha utawala awamu ya tano pia kimeibua maneno ya misimu kama majipu,

hapa kazi tu, hewa, magufulisha, vyuma vimekaza n.k, licha ya mabadiliko ya kiutawala misimu imeibuka kutokana na mabadiliko ya kiutamaduni yameibua maneno kama dingi, marioo, halikadhalika mabadiliko ya kijamii yamesababisha kuibuka maneno ya misimu mfano amsha dude, jaza ujazwe, ukata, mapene, dingi n.k misimu imegawanyika katika aina kuu tatu zagao,pekee na kitarafa na aina zote hizo za misimu zimetokana na madadiliko mbalimbali yanayojitokeza katika jamii, matukio tofauti.

### 5.3.2 Lengo la Pili

Lengo la pili ni kuchunguza kiasi cha matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii utafiti huu umeangalia namna misimu inavyotumika katika mitandao ya kijamii na mtafiti amebaini kuwa matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii inatumika sana na pia watumiaji wa mitandao ya kijamii wanapenda kutumia misimu na watumiaji wanaibua hayo maneno kila wakati kutokana na mabadiliko yanayojitokeza katika jamii au matukio mbalimbali pia matumizi haya yanategemea uzito wa jambo linalozungumzwa na linagusa vipi watumiaji wa mitandao mfano mubashara linatumika kwenye mitandao na vyombo mbalimbali vya habari likimaanisha uhakika au ubora wa jambo. Mtafiti amebaini pia matumizi haya ya misimu katika mitandao ya kijamii watumiaji huwa na lengo la kupunguza hadhira wanayowasiliana nayo hasa pale kundi moja linapotumia misimu ambayo kundi lingine hawawezi kuelewa kwa haraka hivyo matumizi ya misimu katika mitandao ya kijamii hutenga baadhi ya watu katika mawasiliano. Mtafiti amebaini pia misimu inatumika kuficha ukweli wa jambo linalozungumziwa mfano msimu amsha dude watumiaji hutumia msimu huu

kumaanisha kuzungumzia jambo ambalo linagusa tabaka tawala au watu ambao si rahisi kuwazungumzia kiuwazi. Licha ya mtafiti kuweza kubaini kiasi cha utumizi wa misimu katika mitandao ya kijamii pia mtafiti alikusanya orodha hakiki ya hayo maneno ya misimu yanayotumika katika mitandao ya kijamii na maana zake kama kiambatisho Na 01 kinavyoonyesha.

### 5.2.3 Lengo la Tatu

Lengo la tatu ni kubaini changamoto za kutumia maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii katika lengo hili mtafiti ameweza kubaini changamoto za kutumia misimu katika mitandao ya kijamii ambazo ni:

(i) Inaharibu lugha kwa kuwa matumizi ya hayo maneno sio sanifu mfano wa hayo maneno ni dingi,jazwa ujazwe

(ii) Inasababisha ugomvi mfano msimu joka la kibisa kutokana na mbaadhi ya misimu kuwa na maneno makali au ya matusi

(iii) Inaongeza chumvi misimu kama ‘mishe’ ‘shilawadu’

(iv) Kuharibu matumizi ya lugha mfano neno jipu liinamaana tangu awali lakini kwasasa ilikitumiwa linamaanisha watu mafisadi,wahujumu uchumi

(v) Kutumia lugha ya matusi mfano wa misimu boya,shoga neno hili la msimu linamaana ya kawaida rafiki lakini kwa sasa mwanaume akimuita mwanaume mwenzie shoga huwa ni tusi

(vi) Maneno mengine huzuka na kutoweka mfano wa hiyo misimu ni ‘kicheche’ ‘shangingi’ ‘wahenga’‘watu wasiojulikana’ kupitia majadiliano wakufunzi na wahadhiri waliweza kubaini maneno mengine yaliyoweza kuzuka na kutoweka au kupungua kasi ya matumizi yake kupitia mitandao ya kijamii

(vii) Kutoeleweka mfano misimu kama ‘mshua’ ‘dingi’ misimu hii yote ina maanisha mzazi wa kiume hivyo wakati wa majadiliano watafitiwa waliona kuwa misimu hii inaweza isieleweke vizuri kwa kuwa haya maneno yote mawili yana maana moja.

(viii) Kutumia muda mwingi kubuni

(ix) Utoaji wa taarifa kutokuwa sahihi

(x) Lugha kuonekana ya kihuni

(xi) Kutukuelewana katika mitandao

(xii) Kutoa tafsiri isiyo sahihi

(xiii) Kuharibu mahusiano ya jamii

(xiv) Lugha kutofahamika katika eneo kubwa

(xv) Kupata mkanganyiko wa kile kilichokusudiwa na mwandishi

(xvi) Kushindwa kujieleza kwa lugha fasaha

(xvii) Misimu inaleta matabaka

(xviii) Hupunguza hadhira katika mitandao,hutengua mawasiliano, maneno yasiyoaminika katika jamii

(xix) Kubomoa mahusiano baina ya watu

(xx) Lugha ya matusi

(xxi) Kupoteza muda

(xxii) Kushindwa kupata maana halisi ya misimu inayotumika mfano Serengeti boys, marioo.

## 5.4 Hitimisho

Utafiti huu unamchango mkubwa sana kwa watumiaji na wapenzi wa lugha ya Kiswahili kwanza unasaidia kupamba lugha kwa kuwa unaongeza misamiati

katika lugha ya Kiswahili baada ya hii misimu kutumika kwa muda mrefu na kukubaliwa kutumika kama misamiati husika ya lugha ya Kiswahili pili ni chachu kwa wana lexikografia kuweza kupata maneno mapya ambayo watayatumia katika utunzi wao wa kamusi. Utafiti huu utasaidia wageni au wajifunzaji wapya wa lugha ya Kiswahili kufahamu kuwa lugha ya Kiswahili pia inamisimu na maneno hayo sio rasmi hivyo hutumika na kueleweka kwa watu ambao wanaifahamu misimu husika. Mchango mwingine wa utafiti huu ni kuwasaidia watumiaji wa mitandao ya kijamii kufahamu kuwa maneno mengi yanayotumika katika mitandao ya kijamii ni misimu hivyo wanapokutana nao katika ujumbe wowote wanapaswa kutafuta maana ya hayo maneno ilikuweza kuelewa ujumbe husika. Utafiti huu ulikuwa na lengo la kubaini misimu na changamoto zinazojitokeza katika mitandao ya kijamii. Utafiti huu umebaini kuwa misimu ni maneno yanayoibuka na kujitokeza katika jamii kama na kutumika katika mawasiliano na kundi dogo au kubwa la watu. Aidha utafiti huu umebaini kuwa misimu hujitokea katika jamii kulingana na matukio yanyotukia katika jamii au historia ya jamii. Hata hivyo kuna

## 5.5 Mapendekezo

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na watafitiwa kwa kujibu swali lililokuwepo katika dodoso nini kifanyike ili watumiaji wa mitandao ya kijamii waweze kuelewa dhana za misimu katika mawasiliano, na pia mapendekezo haya yametokana na swali la majadiliano baina ya wakufunzi na wahadhiri pamoja na mtafiti lililohusu mapendekezo yanayoweza kutatua changamoto za kutumia misimu katika mitandao ya kijamii:

(i) Watu waelimishwe kuhusiana na matumizi ya misimu

(ii) Kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii

(iii) Kuhifadhiwa kwa misimu na kurasimishwa

(iv) Maneno yanayotumiwa na idadi kubwa ya watu yasanifiwe

(v) Kufuatilia maana ya matumizi ya maneno husika

(vi) Kuwepo na wataalamu wa uchambuzi wa maneno hayo

(vii) Kutumia lugha kwa usahihi

(viii) Watumie misimu inayoeleweka na watu wengi ili iweze kusanifiwa

(ix) Mitandao ya kijamii iwe na program itakayohakiki matumizi sahihi ya lugha husika

(x) Kutoa elimu hasa kwa vijana juu ya namna ya kutumia misimu

(xi) Misimu inayotumika zaidi kutolewa maana.

(xii) Elimu itolewe kabla ya matumizi ya misimu husika vilevile sheria ya mtandao izingatiwe kwa watumiaji

(xiii) Kuhifadhiwa kwa misimu na kurasimishwa.

(xiv) Kuwa wafuatiliaji wa misimu hiyo ili kuweza kujua maana halisi na maana inayobadilishwa

## 5.5 Maeneo Yanayohitaji Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulikuwa unachunguza chanzo cha utokeaji, matumizi na changamoto za kutumia maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii maeneo yanayohitaji utafiti zaidi ni kama vile:

(i) Kuchunguza kwanini rika la vijana na umri wa kati wanapendelea zaidi kutumia misimu wakati wa kuwasiliana kupitia mitandao ya kijamii.

(ii) Kufanya tafiti nyingine za matumizi ya misimu kupitia magazeti au vyombo vingine vya mawasiliano.

# MAREJELEO

Almasi, A. (2011). *Mchango wa Muziki wa Hip Hop Katika Kukuza Kiswahili*, Dodoma: UDOM.

Babbie, E. (1992). *The practice of Social Research*, Calfonia: Wadsworth Publishing Company.

BAKITA, (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Longhorn Publishers (T) Ltd.

Batibo, H. M. (1992). *The fate of Ethics languages in Tanzania*, In M. Brenzinger (ed). Language death: Factual and theoretical explorations, with special reference to East Africa.

Batibo, H. M. (2000). "*The sounds of Africa: Theirphonetic characteristics,* In V. Webb and K. Sure (eds) African voices: An *Introduction to African languages.*

Best, J. W., and Kahn, J. V. (1998). *Research in Education, 8th Ed.* New York: Viacom Company Publishers.

Bukagile, G. R. (2008). *Kiswahili kwa shule za Sekondari; Kidato cha pili,* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publisher.

Chapman R. L. (1995). *Dictionary of American Slang*, New York: Haper Collins Publishers.

Chimera, R. (1998). *Kiswahili Past, present and future Horizons*, Nairobi: OUP.

Cohen, L. (2007). *Research methods in Education, 6th Ed.* London: Routledge Falmer.

Creswell, J. W. (2014) *Research Design: Qualitative, Quantitative and mixed methods approaches*, 4th Ed. California: Sage Publications, Inc

Dalzell, T. (2006). *Power of Slang,* London: Oxford University Press.

Fishman, J. A. (1971). *The Sociology of Language, In J.fishman(ed) Advances in the socilogy of language. Vol.1 217-404.* The Hague: Mouton

Giles, H. (1979). *''Ethinicity Markers in Speech'' In K.R Scheres and H.Giles (eds), Social maker in speech*. London: Cambridge University Press.

Gilham, B. (2004). *Case Study Research Methods,* London: Continuum.

Gronlund, N. E., and Lin, R. L. (1990). *Measurement and Evaluation in Teaching,* New York: Macmillan Publishers.

Hudson, R. A. (1985). Social linguistics, London: Cambridge University Press.

Hymes, D. (1971). *On communicative competence*, Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Hymes, D. (1964). *Language in Culture and Society,* New York: Oxford University Press.

Ibrahim, A. (2012). *Matumizi ya Misimu ya vijiweni Katika lugha ya kiswahili, ''mifano katika Jiji la Dar es salaam''*, Dar es Salaam: UDSM.

Kihombo, M. (2013). *Matumizi ya mtindo wa mawasiliano yasiyo rasmi kwa lugha ya Kiswahili katika redio*. Dar es Salaam: UDSM.

King'ei, K. (1999). "*The Challenge of the Sheng Phenomena in Kenya"* Unpublished Paper Presented at the ATWS Conference, Egerton University, Njoro, Kenya.

King'ei, K. (2010). *Misingi ya Isimu jamii*, Dar -es- Salaam: Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili.

King'ei. K., na Kobia, J. (2007). Lugha kama Kitambulisho. Changamoto ya Sheng nchini Kenya: *Nordic Jornal of African studies, 16(3),* 34 – 41.

Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kipacha, A. (2014). *Misemo Katika Lugha za Magari Divai mpya,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kirkerby W. K. (2002). *English Swahili Dictionary, 2nd Edition*, Norway: Kirkeby Publishing Company.

Kitabu cha Mwanzo (1997). *Biblia, Maandiko Matakatifu,* Dodoma: Bible society of Tanzania.

Kiula, J. (1998). *Kiswahili Slangs,* Dar -es- Salaam: Dar es Salaam University Press.

Kiunga, M. T. (2016). *Maana ya Usemi na Mazungumzo katika mitandao ya Kijamii Hususani Facebook na Twitter,* Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kobia, J. (2006). *"Sheng is not a language but a Popular slang"* katika Sunday nation**,**

Kombo, D. K., and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis writing: Introduction*. Nairobi: Paulines publishers Ltd

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology,* New Delhi:: NewAge International Ltd.

Masebo, J. A., na Nyambari, N. C. (2010). *Nadharia ya Lugha Kiswahili 1*, Dar es Salaam: Nyambari NyangwinePublisher.

Masebo, J. A., na Nyangwine, N. (2002). *Maendeleo ya Kiswahili, Fasihi, sarufi, matumizi, Utungaji na Ufahamu.* Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.

Massamba, D. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha,* Dar es Salaam: TUKI

Mekacha, R. D. (2011). *Isimu jamii Nadhariana Muktadha wa Kiswahili,* Dar es Salaam: Taasisi za Taaluma za Kiswahili

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu,* Nairobi: Longhorn.

Mligo, E. S. (2012). *Jifunze Utafiti.* Dar es Salaam: Ecumerical Gathering

Mohammed, A. N. (2013). *Matumizi ya lugha tandawazi katika simu za kiganjani, Dar es Salaam:* Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam.

Msanjila, Y. P. (2009). *Isimu jamii Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Msanjila, Y. P. (2011). *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo,* Dar-es-Salaam: TUKI.

Msanjila, Y. P. (2007). "Utumiaji WA Kiswahili Na Lugha za Jamii" Kijinsia nchini Tanzania. *In Nordic Journalof African Studies, 3(6),* 34 – 51.

Msanjila, Y. P. (1983). "Nadharia ya Misimu ya Kiswahili"I.K.R (Seminar Paper): *Nordic Journal of African Studies, 3(6),* 34 – 51.

Msungu, J. (1973). *Swahili Slang,* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Mulokozi, K. (1999). *Tenzi Tatu za Kale,* Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1983). *"Utafiti wa Fasihi Simulizi" katika MULIKA Na. 21 uk 7-9.* Dar es Salaam: TUKI

Mwangomango, J. S. M. (1973). *Swahili Slangs and The Physchology of Dar es Salaam Urban Secondary School.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwansoko, H. (1991). *Mitindo ya Kiswahili Sanifu,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mwansoko, L. (1991). *Miundo ya Kiswahili Sanifu*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press

Ngole, C. (2013). *Lugha Inayotumika Katika Masoko ya Nguo za Mitumba Dar es Salaam*, Dar es Salaam: UDSM.

Njabili, A. F. (1999). *Practical guide for classroom measurement and Testing, The basic essential 3rd Ed*, Dar es Salaam: Mture Educational Publishers

Nkwera, F. (2011). *Tamrini za Fasihi Sekondari na vyuo,* Dar Es Salaam: Kitabu Commercial Printin Co.

Nunuu, A. (2013). *"Matumizi ya lugha tandawazi katika simu za kiganjani, Changamoto Kwa wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Nurse, D. na Philippson, G. (1980). *The Bantu languages of East Africa: A lexicostatistical survey.* In Polome, E. na Hill, C.P. Hill (Wahar.) Language in Tanzania, London: OUP.

Nyarapa, C. (1998). *Isimu,* Peramiho: Ndanda Mission Press.

Ohly, R. (1982). *Misemo ya Kiswahili,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Omari, I. M. (2011). *Concept and Methods In Educational Research,* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook,* washington: Centre for Applied linguistic.

Polome, E. na Hill, C. P. (1980). *Swahili in Tanzania*, London: OUP.

Scott, F. (1994). *The World Book Encyclopedia*, London: World Book Inc

Sengo, T. S. Y. (1973). *Misemo ya Mitaani,* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press

Shayo, I. (2015). *Semi zilizoandikwa katika maeneo ya biashara; uchunguzi kuhusu asili, Muundo, miktadha, na utokeaji na dhima,* Dodoma: UDOM.

Sigh, K. (2007). *Quantitative Social Research Methods,* India: SAGE Publication

Spears, R. A. (1991). *Slang and Euphemism,* New York: Penguin publishers.

Stufflebeam, D. L. (1972). “The relevance of the CIPP evaluation model for education Accountability”, *SRIS Quarterly, 5(1),* 32 – 45.

Timothy, K. (2016). *Maana Ya Usemi na Mazungumzo katika mitandao ya Kijamii hususani facebook na twitter,* Nairobi: Chuo Kikuu Nairobi.

TUKI, (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha,* Dar –es- Salaam: TUKI.

Walliman, N. (2011). *Research Methods,* London and Newyork: The Basic.

Willian.W., na Stephen, G. (2004). *Research Methods in Education: An introduction,* New Delhi: Person Education Asia Ltd and China light Industry Press.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho Na. I: Orodha Hakiki ya Maneno ya Misimu

Orodha hakiki ya maneno ya misimu maana/matumizi yake ambayo mtafiti ameyakusanya kutoka uwandani na kuyahakiki

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Msela | Kuonyesha urafiki wa karibu na mtu mwingine |
| Dingi | Hutumika kumaanisha baba |
| Mishe | Hutumika kumaanisha shughuli za kila siku |
| Aje | Hutumika kujulia hali |
| Shilawadu | Mtu mmbeya, kusema watu na msengenyaji wa mambo |
| dili | Hutumika kuulizia kazi ya kufanya |
| Demu | Msichana mzuri na mrembo |
| Faza wa nchi | rais |
| Kwa bibi titi | kijijini |
| Kausha | nyamaza |
| Niga | rafiki |
| Kimewaka | kimeharibika |
| Ambushi | nguvu |
| Mbwa wa Nyerere | polisi |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Mkwara | vitisho |
| Povuka | toweka |
| Dope | poa |
| Mshua | baba |
| sepa | ondoka |
| Bi mkubwa | mama |
| swaga | maneno |
| skendo | Taarifa mbaya |
| ubuyu | umbea |
| ushilawadu | Kutafuta umbea |
| mchepuko | Mpenzi wa kimapenzi nje ya mahusiano halali |
| nehemeka | bahatika |
| jipu | udanganyifu |
| Bi mdashi | mama |
| Sir God | Mungu |
| Kicheche | malaya |
| Kigulu na njia | mzululaji |
| Jaza ujazwe | Toa upewe |
| kiki | Kutafuta umaarufu |
| Shikopa | poa |
| Msichana Yule kisu | Msichana mzuri |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Kutupia mavazi | kupendeza |
| Sina swaga | Sina maneno |
| mchepuko | Kuwa na wapenzi wengi |
| kidumu | Mke,mme wa pembeni |
| Blaa blaa | Kufanya kitu kwa kupuuza |
| Sikufagilii | Kutompenda mtu |
| Shoboka | Kutopenda kitu |
| Ngunguli | Wakati wa kampeni |
| Mshua | Jina la kumuita baba |
| Majipu | Kuonyesha watu wasio na sifa |
| kutumbua | Kuachisha kazi au ajira |
| Mchizi | Hutumika kama rafiki |
| Nguvu mpya | Uongozi mpya |
| Wahenga | Watu waloishi miaka mingi |
| Swaga za kibantu | Story za mitaani ambazo huongelewa kijiweni |
| mwanangu | Rafiki au ndugu |
| kausha | nyamaza |
| kiki | Kutafuta sifa |
| jimwage | jiachie |
| mshikaji | rafiki |
| kutext | Ujumbe mfupi |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| niiniboxi | Nitumie ujumbe moja kwa moja |
| Hamsha popo | Kuibua tatizo |
| Hamsha dude | Toa jambo lolote linalowafanya watu wawe makini kufuatilia |
| Mambo meusi | Mambo yasoeleweka |
| Bi mkuda | Mtu mmbea sana |
| nimekusoma | nimekuelewa |
| Mtoto jojo | Maneno maneno |
| Udaku | umbea |
| usonji | Ugonjwa wa kitabia |
| bodaboda | Pikipiki zinazotumika kusafirisha abiria |
| ganja | Madawa ya kulevya, bangi |
| mtoto | Humaanisha msichana kwenye maongezi miongoni mwa wavulana au wanaume |
| kopo | Kutokuwa na akili |
| kilaza | Mtu asiyekuwa na akili |
| modo | Suruali inayobana chini |
| Kamatia chini | Suruali yenye mpira chini |
| bwashe | shemeji |
| mida | baadae |
| kushinei | maliza |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Nifanyie kweli | usiniangushe |
| singeli | Nyimbo za uswahilini |
| Maria Roza | Miguu mirefu |
| jikate | kujiondoa |
| Chanja mbuga | toroka |
| mkwanja | pesa |
| fulia | filisika |
| kidoti | Mwanamke mzuri |
| buzi | Mwanaume wa pembeni |
| jero | Mia tano |
| buku | Elfu moja |
| Bati moja | Mia moja |
| msimbazi | Elfu kumi |
| mshua | baba |
| mchizi | rafiki |
| msimbazi | Elfu kumi |
| boya | mpumbavu |
| mbwembwe | Maelezo mengi yasiyo na maana yoyote |
| madikodiko | Vitu vitamu |
| unga | Madawa ya kulevya |
| ndani | jela |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Mwenye nyumba | Kiongozi wa nchi |
| Kukata kamba | kufa |
| Kiti kikuu | Kiti cha kiongozi |
| Nyumba nyeupe | ikulu |
| Kumwaga unga | Kujiharibia riziki |
| Mwenza wa damu | Ndugu wa karibu |
| Kuvaa miwani | kulewa |
| Njia kuu | Kuwa mwaminifu katika mahusiano |
| kuzingua | Mtu kujiweka kana kwamba haelewi |
| tukunyema | Mwanaume mnene |
| mawaya | Hutumika katika ugonjwa wa ukimwi |
| chakachua | Chukua kitu kisicho halali |
| Fataki | Mwanaume mwenye wapenzi wengi |
| Tozi | Kijana anayejipenda na kwenda na wakati |
| amada | Mlevi kupitiliza |
| Kijogoo wa mtaa | Mvulana Malaya katika mtaa |
| mrupo | Rafiki wa kike malaya |
| Kukwea pipa | Panda ndege |
| Mubashara | Matangazo ya mojakwa moja |
| Dada poa | malaya |
| mwepesi | Kuwa huru |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Joka la kibia | Sio lijali |
| Kupiga dili | Kufanya mipango isiyo halali |
| Bao la mkono | Kushinda jambo kwa kutumia mbinu chafu |
| Chapa ilale | kuondoka |
| masela | marafiki |
| Bampa tu bampa | Moja kwa moja |
| shosti | rafiki |
| Upo nyonyo | unaelewa |
| gumegume | Mwanaume mkorofi |
| Mailkia wa nguvu | Mwanamke shupavu |
| Mwanaume suruali | Wanaume wanaopenda kuhudumiwa |
| chura | makalio |
| Kibenteni | Mvulana mdogo |
| kibendi | Mwanamke mjamzito |
| Ndondo cup | Mpira mchangani |
| Serengeti boys | Mwanaume mdogo kiumri |
| Zege | Chips mayai |
| zombi | Mtu asiyejielewa |
| kudodesha | Kuharibu jambo |
| Gumegume | Mtu mkorofi mwanaume |
| majani | bangi |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| Futa mapesa | Kuwa na pesa |
| mpunga | pesa |
| majuu | Nchi za nje |
| Kudodesha | Kuharibu kitu |
| Amsha popo | kuondoka |
| michongo | harakati |
| mkoko | Nyumba nzuri sana |
| veepe | vipi |
| nitoe | Nitatie fedha/ nilipe |
| manzi | binti |
| kigogo | Mtu mwenye pesa |
| Mshika pembe | Mwanaume anayedanganywa kwenye mahusiano |
| bashite | Aliyefoji vyeti |
| vuvuzela | Mwanamke anayeongea sana |
| zali | bahati |
| mlupo | Rafiki wa kike malaya |
| unoko | umbea |
| kukinikisha | Kuanzisha fujo |
| pipa | Usafiri wa ndege |
| kitololi | kuwadi |
| shalobaro | mtanashati |

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Maana/Matumizi yake** |
|---|---|
| michongo | harakati |
| bingo | kufanikiwa |
| kigogo | Mtu mwenye pesa |
| kitololi | kuwadi |
| mzuka | safi |
| Vyuma vimekaza | Hali ngumu ya upatikanaji wa fedha |
| Kuwa na mawe | Mtu mwenye pesa nyingi |

**Kiambatisho Na. II: Maswali kwa Wahojiwa**

Hojaji hii imeandaliwa na mtafiti kwa lengo la kuwapatia watafitiwa ili waweze kujaza ili kujipatia taarifa na taarifa itakayotolewa itakuwa siri baina ya mtafiti na mtafitiwa.

Weka alama (√)

1. a.Umri wako ni

   b. Kazi yako ni ipi? Mwanachuo [ ] Mwalimu [ ]

2. Unatumia mtandao wowote wa kijamii? Ndiyo/ hapana
3. Je unatumia lugha gani katika mawasiliano yako katika mitandao ya kijamii……….
4. Kama ni lugha unayotumia ni Kiswahili, je unatumia fasaha (yaani Kiswahili ambacho ni sahihi bila makosa) au unatumia Kiswahili chenye makosa (yaani ngeli zinapishana kwa mfano wanamuziki wanaposema *'hii ni nyimbo yangu ya kwanza'* badala ya '*huu ni wimbo wangu wa kwanza'* n.k.) Je jibu lako ni ndiyo/hapana
5. Kuna kitu tunaita 'misimu'. Misimu ni maneno yanayozuka na kutumika katika jamii lakini ghafla hupotea kwa kukosa matumizi. Je, umeshasikia maneno yoyote ambayo unaweza kuyaita misimu? Ndiyo/hapana.
6. Kama jibu ni ndiyo, yataje baadhi ya maneno hayo…………..
7. Je, unapotumia Kiswahili unatumia misimu katika mawasiliano yako?
8. Ni aina gani ya maneno ambayo unapenda kuyatumia zaidi?je ni maneno rasmi (yaani maneno sahihi) au yasiyo rasmi (yaani maneno yasiyo sahihi)? = jaribu kumrahisishia muulizwa maswali kwani maswlai yote yakiwa

magumu atajibu bila kuzingatia ‘ukweli’ bali atalipua ili usimpotezee muda wake. Maswali yote yakiwa magumu yanamvunja moyo. Jaribu kurahisisha kidogo kwa kumpa majibu ya kuchagua au kumfafanulia maana ya ‘maneno’ kwani anaweza asijue au asikumbuke

9. Kwa kiasi gani maneno ya misimuyanatumika katika mitandao ya kijamii?

    a. Kidogo

    b. Sana

    c. Hayatumiki kabisa ( )

10. Fafanua jibu lako kwa ufupi

    ……………………………………………………………………………………

    ……………………………………………………………………………………

11. Unapata changamoto gani kuelewa dhana iliyopo katika maneno hayo ya misimu katika mitandao ya kijamii.

    ……………………………………………………………………..……………………

    ………………………………………………………………………………………

    …………………………………………………………………………………

12. Toa maoni yako kwa kifupi kuhusiana na matumizi ya maneno ya misimu katika mitandao miandao ya kijamii

    ……………………………………………………………………………………

13. Mtindo wa kutumia misimu katika mitandao ya kijamii una athari gani katika lugha? Taja unazojua……………………………………………………….

14. Misimu inaathiri vipi mawasiliano katika mitandao ya kijamii? Toa maoni yako

…………………………………………………………………………..

…………………………………………………………………………

………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………

15. Ni rika gani hasa hupendelea kutumia misimu,weka alama katika miaka ifuatayo.

    a) Miaka 12-35 ( )
    b) Miaka 35-45 ( )
    c) Miaka 45-60 ( )

16. Ni kwa sababu gani rika hilo hupendelea kutumia misimu katika mitandao ya kijamii.

    i. …………………………………………………………………
    ii. …………………………………………………………………
    iii. …………………………………………………………………
    iv. …………………………………………………………………

17. Changamoto zipi zinazowakabili watumiaji wa mitandao ya kijamii wanapotumia misimu.

    a) …………………………………………………………………
    b) …………………………………………………………………
    c) …………………………………………………………………
    d) …………………………………………………………………

18. Nini kifanyike ili watumiaji wa mitandao ya kijamii waweze kuelewa dhana iliyomo katika misimu inayotumika katika mawasiliano. (Toa ushauri wako)

…………………………………………………………………….

**Kiambatisho Na. III: Orodha Hakiki ya Kupata Maneno ya Misimu**

Orodha hakiki itatumika na mtafiti kupata orodha ya maneno ya misimu pamoja na matumizi yake katika mitandao ya kijamii kutoka kwa watafitiwa wanachuo.

| **Orodha ya maneno ya misimu** | **Matumizi ya hayo maneno** |
|---|---|
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |
| | |

**Kiambatisho Na. IV: Maswali kwa Wahojiwa**

Maswali ya majadiliano

Mtafiti atatumia Mahojiano na wakufunzi wanaofundisha masomo ya lugha katika Chuo cha Ualimu Morogoro, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro, sababu ni walimu wa somo la Kiswahili hivyo wanauelewa wa kutosha na somo la Kiswahili pia wanauzoefu wa kufundisha somo hilo ili kuweza kupata chanzo, matumizi na changamoto ya maneno ya misimu katika mitandao ya kijamii.

Misimu ni maneno yanayoibuka na kutoweka kulingana na mabadiliko ya kijamii, kiutamaduni, kisiasa huwa yanaweza kutumika kwa muda mrefu na yakasanifishwa kuwa maneno sanifu ya lugha maneno mengine huzuka na kutoweka. Mfano wa misimu shangingi, boya.

1. Unaelewa nini kuhusu mitandao ya kijamii.
2. Unaelewa nini kuhusu chimbuko la misimu.
3. Unatumia misimu katika mitandao ya kijamii? Kwa kiasi gani?
4. Je misimu ina faida yoyote katika mawasiliano yako katika mitandao ya kijamii. Kama jibu ni ndiyo zitaje ……………………………………
5. Changamoto unazokumbana nazo wakati unatumia misimu katika mitandao ya kijamii.
6. Taja mapendekezo yanayoweza kutatua changamoto za kutumia misimu katika mitandao

**Kiambatisho Na. V: Kibali cha Utafiti (MUM)**

**Kiambatisho 05: Kibali cha Utafiti (MUM)**

The Open University of Tanzania
Morogoro Regional Centre
Plot 680 Block J
Barakuda - Mazimbu

P.O. Box 2062
Tel.No: 023 2613303
MOROGORO, TANZANIA

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Kituo cha Morogoro
Plot 680 Block J
Barakuda – Mazimbu

S.L. Posta 2062
Simu Na. 023 2613303
MOROGORO, TANZANIA

28 June 2017

Ref. No. OUT/MOR/SC/P/I/Vol.1/90

Head Department of Kiswahili
Muslim University
P.O. Box 1031
Morogoro

Received
She is allowed to conduct her survey.
4 HOD OKS 14/07/2017

RE: Introduction of Ms. Malima Christina Clement Reg. No. PG201507135 (MA Kiswahili) Student

The individual named above is a student in the Master of Arts in Kiswahili (MA Kiswahili) programme of the Open University of Tanzania studying at Morogoro Regional Centre.

The student is interested in conducting Research titled **"Kuchunguza Matumizi ya Misimu kwenye Mitandao ya Kijamii kwa Wazungumzaji wa Lugha ya Kiswahili Vyuoni Morogoro"** for the fulfillment of the requirements of the programme of study.

I would appreciate if you could allow and provide the necessary environment for the students to carry out the exercise satisfactorily within the region.

We thank you in advance for your cooperation and continued support.

Yours sincerely,

Dr. Wambuka Rangi
Director of Morogoro Regional Centre

CC. Ms. Malima Christina Clement

Cell: 0713 454296 | Email: *drcmorogoro@out.ac.tz*

**Kiambatisho Na. VI: Kibali cha Kufanya Utafiti (Mhanda TC)**

The Open University of Tanzania
Morogoro Regional Centre
Plot 680 Block J
Barakuda - Mazimbu

P.O. Box 2062
Tel.No: 023 2613303
MOROGORO, TANZANIA

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Kituo cha Morogoro
Plot 680 Block J
Barakuda – Mazimbu

S.L. Posta 2062
Simu Na. 023 2613303
MOROGORO, TANZANIA

13 July 2017

Ref. No. OUT/MOR/R/P/I/Vol.1/85

Principal
Muhonda Teachers' College
P.O. Box 14
Turiani

Received on 18th July, 2017
Plse Academic Dean respond to the issue.
FOR PRINCIPAL
MHONDA TC
TURIANI

RE: Introduction of Ms. Malima Christina Clement Reg. No. PG201507135 (MA Kiswahili) Student

The individual named above is a student in the Master of Arts in Kiswahili (MA Kiswahili) programme of the Open University of Tanzania studying at Morogoro Regional Centre.

The student is interested in conducting Research titled **"Kuchunguza Matumizi ya Misimu kwenye Mitandao ya Kijamii kwa Wazungumzaji wa Lugha ya Kiswahili Vyuoni Morogoro"** for the fulfillment of the requirements of the programme of study.

I would appreciate if you could allow and provide the necessary environment for the students to carry out the exercise satisfactorily within the region.

We thank you in advance for your cooperation and continued support.

Yours sincerely,

Director
Morogoro Regional Centre
Open University of Tanzania
P.O. Box 2062, Morogoro

Ms. Divine Mwaluli
For Director of Morogoro Regional Centre

CC. Ms. Malima Christina Clement

## Kiambatisho Na. VII: Kibali cha Kufanya Utafiti (Morogoro TC)

The Open University of Tanzania
Morogoro Regional Centre
Plot 680 Block J
Barakuda - Mazimbu

P.O. Box 2062
Tel.No: 023 2613303
MOROGORO, TANZANIA

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
Kituo cha Morogoro
Plot 680 Block J
Barakuda – Mazimbu

S.L. Posta 2062
Simu Na. 023 2613303
MOROGORO, TANZANIA

28 June 2017

Ref. No. OUT/MOR/SC/P/I/Vol.1/90

Principal
Morogoro Teachers College
P.O. Box 691
Morogoro

permitted/offered access
11/7/2017

MKUU WA CHUO ... MOROGORO
S.L.P. ... MOROGORO

RE: Introduction of Ms. Malima Christina Clement Reg. No. PG201507135 (MA Kiswahili) Student

The individual named above is a student in the Master of Arts in Kiswahili (MA Kiswahili) programme of the Open University of Tanzania studying at Morogoro Regional Centre.

The student is interested in conducting Research titled **"Kuchunguza Matumizi ya Misimu kwenye Mitandao ya Kijamii kwa Wazungumzaji wa Lugha ya Kiswahili Vyuoni Morogoro"** for the fulfillment of the requirements of the programme of study.

I would appreciate if you could allow and provide the necessary environment for the students to carry out the exercise satisfactorily within the region.

We thank you in advance for your cooperation and continued support.

Yours sincerely,

Dr. Wambuka Rangi
Director of Morogoro Regional Centre

CC. Ms. Malima Christina Clement

Cell: 0713 454296 | Email: *drcmorogoro@out.ac.tz* 1